Siasa

## Kuondoka Nchimbi kwafungua maswali magumu zaidi

Uk. 20

Siasa

## OMO awapa wawakilishi jukumu zito



Uk. 16

Mzee Tai



## Naogopa Mungu, teknolojia na sasa CCM

Safu Uk. 5


# Pambazuko


Toleo Namba 180 Jumatatu, Agosti 31-Septemba 6, 2026


## El-Nino yashtua serikali, mikakati yaanza kukabili

Uk. 14

# Mizizi historia ya Ndejembi

Uk. 6&7



Deogratius



Deogratius akiwa na mama yake, Amina

## Tundu Lissu alivyohitimisha mchuano wa ushahidi mahakamani


**MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amehitimisha safari ya siku tano ya kuwasilisha ushahidi wake binafsi, katika kesi ya uhaini inayomkabili.**

Habari Uk. 12

Tafakuri ya Bagonza

## Ukakasi na uhaini mamboleo

Safu Uk. 10



# Utata alipo Dkt Nchimbi

Habari Uk. 8&9

Scanned with MOBILE SCANNER

Tahariri

# Ndejembi, kasimamie ustawi wa Tanzania, amani

TUNAMPONGEZA Deogratius John Ndejembi kwa kuaminiwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kuapishwa kwake Ikulu ya Chamwino, Dodoma, Agosti 29, 2026, baada ya kuthibitishwa kwa kauli moja na wabunge 324, ni mwanzo wa jukumu zito linalohitaji hekima, uadilifu na uzalendo usiotetereka.

Rais Samia Suluhu Hassan alimshauri akue katika hekima, siyo umri pekee. Ushauri huo una maana kubwa. Nafasi ya Makamu wa Rais siyo ya mapambo, makofi wala kufuata upepo.

Katiba ya Tanzania inamtaja yeye ni msaidizi mkuu wa rais, anayepaswa kumshauri kwa uaminifu na kusaidia kufuatilia utekelezaji wa shughuli za serikali.

Ndejembi anaingia madarakani katika kipindi ambacho Watanzania wanataka maendeleo yanayoonekana, haki inayotendwa na usalama usiochagua.

Sisi Pambazuko tunamtaka atumie nafasi yake kumweleza rais ukweli, hata pale ukweli huo unapokuwa mchungu. Taifa halihitaji wasaidizi wanaosema "ndiyo" kwa kila jambo; linahitaji viongozi wanaotambua hatari mapema na kushauri kwa maslahi ya nchi.

Tunamtahadharisha ajilinde dhidi ya makundi ya watu wanaoweza kumzunguka kwa sifa, majungu na ushauri wenye sumu.

Wapo wanaotumia ukaribu na viongozi kujitajirisha, kuwakandamiza wenzao, kulipiza visasi na kuficha maovu. Watu hao hujivika ngozi ya uzalendo huku wakitafuna misingi ya taifa.

Ndejembi asikubali ofisi yake kuwa daraja la wala kivuli cha wanaotaka kukwepa uwajibikaji.

Zaidi, Ndejembi anapaswa kuwa sauti thabiti dhidi ya utekaji, kupotezwa kwa watu, mateso na matumizi mabaya ya mamlaka.

Aidha, atambue kuwa amani ya Tanzania haiwezi kujengwa juu ya hofu au ukimya wa familia zisizojua walipo wapendwa wao, akahimize kila madai ya kupotea kwa mtu yachunguzwe kwa uwazi, wahusika wawajibishwe na vyombo vya dola vikumbushwe kuwa wajibu wao ni kulinda maisha na haki za wananchi.

Ndejembi pia akaonyeshe kuwa rushwa bad oni adui mkubwa wa taifa, akamshauri rais kuongeza mapambano kuiomomeza.

Tunahimiza zaidi Ndejembi asaidie kusimamia matumizi ya fedha za umma, miradi ya maendeleo, zabuni na uwajibikaji wa watendaji.

Pia, aunge mkono kwa dhati ya moyo wake, taasisi za uchunguzi na kamwe asitetee mtu kwa sababu ya urafiki, chama, cheo au utajiri. Atambue kuwa kwenye rushwa ama fedha zinapoibwa, maana yake Watanzania wanaporwa.

Awe daraja kati ya serikali na wananchi, Tanzania Bara na Zanzibar, watawala na wakosoaji. Asikilize vijana, wanawake, wafanyakazi, wakulima, wafanyabiashara, viongozi wa dini, wanahabari na asasi za kiraia.

Ndejembi ajenge Imani kwamba kukosolewa siyo kuchukiwa; mara nyingi ni nafasi ya serikali kuona ilipokosea kabla tatizo halijawa kubwa.

Pia, asimamie kwa karibu ajenda za mazingira na Muungano, ambazo ni miongoni mwa majukumu nyeti ya ofisi yake. Maendeleo yasiharibu vyanzo vya maji, ardhi na maisha ya wananchi, wala tofauti za Muungano zisiachwe kukua kwa ukimya mrefu.

Ndejembi ana nafasi ya kujenga urithi wa kiongozi aliyekuwa mwaminifu kwa rais bila kuisaliti dhamira ya taifa. Uaminifu wa kweli siyo kuficha makosa, bali kuyasema mapema na kusaidia kuyarekebisha.

Tunamtakia mafanikio, lakini tunamkumbusha; makundi hupita, vyeo huisha, na sifa hunyamaza, sasa akatende kazi kuwatumikia Watanzania.

Scanned with MOBILE SCANNER

# Kilio cha Wafanyabiashara



*Wafanyabiashara wa Manzese-Midizini wakiwa wamepanga bidhaa zao chini baada ya mabanda yao kubomolewa ili kupisha ujenzi wa barabara ya Midizini ambayo ilikuwa inapitika kwa shida kutokana na msongamano wa watu na bidhaa zilizopangwa kiholela na kusababisha watembea kwa miguu na vyombo vya moto kupita kwa taabu. (Picha na Pambazuko).*


## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **"HABARI"** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **"HABARI"** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**



## TIMU YA PAMBAZUKO

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Mhariri Mkuu** | : | Simon **MKINA** | (simon@pambazuko.or.tz) |
| **Mhariri Mtendaji** | : | Peter **NYANJE** | 0784 211 716 |
| **Mwandishi Mkuu** | : | Elizabeth **HOMBO** | 0712 792 216 |
| **Mwandishi Mwandamizi** | : | Andrew **MSECHU** | 0769 415 815 |
| **Mkuu wa DTP** | : | Yassin **LUPATU** | 0782 009 971 |
| **Mkuu wa Utawala** | : | Tryruckia **MFINANGA** | 0744 768 263 |

***Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A – nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz***


Scanned with MOBILE SCANNER

# Dunia: Hapa na Pale

## Waamua kuvaa kaptula ofisini

WAFANYAKAZI nchini Japan wameanza kuvaa kaptula ofisini, ili kukabiliana na majira ya joto kali la kiangazi nchini humo.

Katika mji mkuu wa Japan, Tokyo, kampeni ya muda mrefu ya serikali ya jiji la Tokyo inayohimiza wafanyakazi kutovaa tai na makoti, imekosa nguvu na sasa wafanyakazi wanahimizwa kuacha kuvaa suruali ndefu na hata kujaribu kuvaa fulana na viatu vya michezo.

Kadiri joto linavyozidi kuikumba Ulaya, wafanyakazi wengine wameanza kuiga mfano wa Tokyo, wakati mwingine kwa kuungwa mkono na mamlaka za waajiri, na maeneo mengi wameanza kuunga mkono.


## Maafa Nepal na China

MAAFA yanayotokana na mafuriko huko Nepal na China, yanatajwa kusababisha zaidi ya vifo vya watu 633 na wengine zaidi ya 3,000 kupotea, huku waokoaji wakiendelea kutafuta miili katika vijiji vinavyozunguka eneo la Himalaya mpakani wa nchi hiyo na Tibet.

Mafuriko hayo ya ghafla yameripotiwa kusomba vijiji baada ya mvua ambazo hazikutarajiwa. Kwa upande wa Tibet, watu saba wameripotiwa kufariki dunia na wengine 554 hawajulikani walipo.

Takwimu zinaeleza idadi ya waliopotea nchini Nepal inaendelea kuongezeka, baada ya mamlaka kuongeza wafanyakazi 933 wa miradi ya kuzalisha umeme kwa maji katika orodha hiyo.

Watalii, wafanyakazi wa kigeni na mahujaji waliokuwa wakielekea Mlima Kailash nchini Tibet pia ni miongoni mwa waliopotea.



## Wahuni wazidi kumvuruga Ruto

RAIS William Ruto anaendelea kukabiliana na vizingiti kutoka kwa makundi ya wahuni wanaotaka kukwamisha kampeni yake ya kurejea madarakani katika uchaguzi mkuu mwakani, baada ya fujo zilizosababisha majeruhi kadhaa katika Kaunti ya Narok mwishoni mwa wiki.

Ghasia za kisiasa zilizoibuka kwa watu wenye mishale kuvamia katika kituo cha biashara cha Mamboleo kabla ya hafla ya rais kuanza, zilitia doa ziara yake, hali iliyomlazimu Ruto kuwakemea viongozi hasimu hadharani na kuwataka kumaliza tofauti zao za kisiasa mara moja.

Mapigano hayo yalihusisha wafuasi wa Mbunge wa Emurua Dikirr, David Keter na mpinzani wake wa kisiasa Bernard Ng'eno ambao walikabiliana kwa kutumia silaha kali ikiwemo mishale.



## Muhoozi avuruga mashemeji

MKUU wa majeshi ya Uganda, Jenerali Kainerugaba Muhoozi, ameibua mzozo wa kifamilia baada ya kumkashifu hadharani shemeji yake, Drek Rwabwogo, ambaye ni mume wa askofu Patience Museveni Rwabogo.

Katika mzozo huo ambao umetokea hadharani, Jenerali Muhoozi alitishia kimkamata shimeji yake huyo, huku akisema kwamba atazungumza na dada zake wawili, Patience na Natasha kutatua mzozo uliopo.

Jenerali Muhoozi ambaye pia ni mtoto wa Rais Yoweri Museveni aliandika katika mtandao wa X, akizungumza kwa ukali kuhusu shimeji yake huyo ambaye pia ni mshauri mwandamizi wa Rais Museveni na mwenyekiti wa Kamati inayoshughulikia mauzo ya nje na maendelo ya kiviwanda nchini Uganda (PACEID).

Scanned with MOBILE SCANNER

Na Mzee TAI

# Naogopa Mungu, teknolojia na sasa CCM

NINA hofu tatu kubwa katika maisha. Namwogopa Mungu. Naiogopa teknolojia. Na sasa, nakihofia Chama Cha Mapinduzi—CCM.

Lakini hofu hizi hazifanani, Mungu namwogopa kwa uchaji. Namwabudu. Nampa heshima yake. Najua anaona ninapotenda mema na ninapojifanya mwema kwa sababu kamera ipo karibu.

Mungu hahitaji taarifa ya Kamati Kuu. Hajadiliani na wajumbe. Hukumu yake haina kikao cha dharura wala taarifa kwa vyombo vya habari.

Teknolojia nayo naiogopa. Hii ni "kiumbe" kisicholala. Unazima simu, minara inakumbuka ulipokuwa. Unakana sauti yako, wataalamu wanaipima. Unaficha picha, mtu tayari amepiga "screenshot." Teknolojia haina huruma kwa siri iliyolelewa kwa miaka. Huivua nguo hadharani, kisha inaiwekea tarehe, saa na mahali.

Zamani mtu angeweza kusema, "Sikuwahi kutamka hivyo." Leo video inamjibu kabla hajamaliza sentensi, hata kama anaweza kudai imenakiliwa vibaya. Simu ndogo inakuwa shahidi mkubwa. Hakuna kiapo. Hakuna hongo. Inakumbuka tu.

Sasa nimeongeza CCM kwenye orodha.

CCM ni chama kikongwe. Kimejengwa na watu. Kimebeba watu. Kimewalea, kimewapandisha na kuwapa majina makubwa, lakini usidanganyike. Chama kinaweza kumgeukia hata fundi aliyesaidia kujenga ukuta wake. Leo unaweka tofali. Kesho ukuta unakuzibia mlango.

Ukikizengua, kinakuzengua mara mia. Wewe una hoja moja; chenyewe kina kamati saba. Una barua; kina katiba, kanuni, taratibu na msemaji mwenye uso usiosoma huruma. Unasema unaondoka mwenyewe. Chama kinakuwahi kutangaza kwamba kimekuondoa. Unataka kuaga kwa heshima. Kinaongeza muhuri wa nidhamu kwenye koti lako.

Hatari sana chama hiki, yaani kinaweza kukupa gari, walinzi na jukwaa, halafu siku moja kikakuachia kiti. Waliokuwa wakikuita "mheshimiwa" huanza kuuliza kama kweli walikuwa wanakufahamu.

Picha zako zinaondolewa ukutani kwa kasi ambayo hata teknolojia yenyewe inaweza kuionea wivu. Jana ulikuwa historia. Leo umekuwa tahadhari hai.

Ndani yake, cheo kinaweza kuwa mwavuli wakati wa jua na radi wakati wa mvua, leo wanakupigia kofi. Kesho kofi inakuwa kura ya kauli moja ya kukutoa.

Waliokuita "jembe la chama" wanaweza kugundua ghafla kwamba jembe hilo limepinda. Hakuna anayekumbuka mashamba uliyolima. Wote wanakumbuka ulipokataa kuchimba walipotaka.

CCM ina kumbukumbu ndefu kuliko simu. Ina masikio mengi kuliko teknolojia. Ina macho yanayoweza kuona mkutano ambao hukuitisha na kusikia maneno ambayo hukuyasema hadharani.

Ukikaa kimya, wanatafsiri ukimya. Ukizungumza, wanapima sauti. Ukicheka, wanauliza ulicheka na nani. Ukikosa kucheka, wanafungua faili.

Ndiyo maana naiogopa, lakini hofu yangu siyo ibada. Mungu pekee ndiye anayestahili kuabudiwa. Teknolojia inapaswa kueleweka na kutumiwa kwa busara.

Chama kinapaswa kuheshimiwa, kuhojiwa na kukumbushwa kwamba nacho kimeundwa na binadamu. Hakipaswi kuwa miungu ya kisiasa.

Tatizo huanza chama kinapotaka utii kuliko ukweli. Mwanachama anapolazimika kuchagua kati ya dhamiri na kadi, taifa hupoteza. Chama kinakuwa salama, lakini siasa zinakuwa wagonjwa.


CCM naiogopa nikitazama historia yake. Mungu husamehe anayeomba. Teknolojia wakati mwingine husahau baada ya "update." Lakini CCM, mhhh! Hicho kinaweza kukumbuka kosa ambalo hata wewe hukujua umetenda.

Usikizengue. Utazengu[illegible]a kwa kauli moja.

Scanned with MOBILE SCANNER

Habari Kuu

# Mizizi historia ya Ndejembi



Deogratius

Na Waandishi WETU

DEOGRATIUS John Pancras Ndejembi, aliyeapishwa Agosti 29, 2026 kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania, amefika katika nafasi ya pili kwa mamlaka nchini akiwa na miaka 43.

Baada ya kuapishwa, mmoja wa wanafamilia yake alisikika akitamka; "Masonrnyii Deo," – neno la Kigogo lenye maana ya "hongera."

Kupanda ngazi katika utumishi na hata kazini, kumekuwa kwa kasi; kutoka sekta binafsi, miundo ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), ukuu wa wilaya, ubunge na uwaziri hadi Ikulu.

Wasifu unaorejelewa na Bunge unataja Julai 12,1983 kuwa tarehe yake ya kuzaliwa, huko Moshi, Kilimanjaro.

Kinachothibitika zaidi ni kuwa ukoo wa Ndejembi, upande wa baba yake, una mizizi eneo la Mkonze, Dodoma, ambako mwanasiasa mkongwe Pancras Mtemi Ndejembi alizikwa Januari 2019.

Baba yake makamu wa rais ni John, huku Pancras akiwa babu yake upande wa baba.

Pancras ndiye kiungo kikubwa kinachoeleza mazingira ya kisiasa aliyokulia Deogratius.

Aliiongoza CCM Mkoa wa Dodoma kwa miaka 25, kuanzia 1982 hadi 2007, na pia akawa mwenyekiti wa wenyeviti wa CCM wa mikoa. Alifariki Desemba 29, 2018 katika Hospitali ya Rufaa ya Dodoma.

Taarifa za mazishi zilisema aliacha mjane, watoto 13 na wajukuu 24, ishara ya ukoo mkubwa uliokuwa na mizizi na ushawishi mkoani Dodoma.

Tofauti na Pancras, historia ya kazi na maisha ya John, ambaye ni baba yake makamu wa rais, haijaandikwa kwa kina katika kumbukumbu zilizopo.

Hata hivyo, Pambazuko linaweza kueleza pasina shaka kwamba baba yake Deogratius, aliishi Moshi kwa muda na ndiko alipokutana na Amina na kuanza uhusiano na hatimaye kupatikana kwa mtoto ambaye sasa ni makamu wa rais.

Baadaye, John alirejea Dar es Salaam akiendelea na maisha na shughuli zake, na kuishi nyumba za Msajili, eneo la Fire, Dar es Salaam.

Deogratius aliishi na baba yake kwa muda kabla ya kupelekwa Dodoma kwa babu yake ambapo alikulia, kusoma elimu ya awali nyumbani, msingi na sekondari kabla ya kwenda Uingereza kwa elimu ya juu.

**Ukoo wa mama yake**

Mama yake Deogratius, anaitwa Amina Shariff Mudhari, ambaye alizaliwa Moshi na kukulia huko kabla ya kwenda Uingereza kwa ajili ya masomo na kuanza kazi.

Inaendelea Uk. 7

Scanned with MOBILE SCANNER

# Mizizi historia...

Inatoka Uk. 6

Babu yake Deogratius alikuwa mmoja wa waanzilishi wa Uislam mkoani Kilimanjaro na alikuwa miongoni mwa wafanyabiashara na mwalimu wa elimu ya Kiislam kwa miaka mingi. Alifariki na kuzikwa Moshi kwenye makaburi ya Mbuyuni. Bibi yake aliitwa Khadija Mudhari.

Familia ya Deogratius hukutana mara kwa mara kwa ajili ya ibada na kuzulu makaburi ya ndugu zao ambao wengi wamezikwa alikozikwa babu yao.

### Kuitafuta elimu

Safari ya elimu ya Ndejembi ilianza Cannon Andrea, iliyoko Dodoma - Mwaka Primary School kati ya 1988 na 1995.

Aliendelea Sekondari ya Jamhuri na Kigurunyembe, kisha Merton College kwa elimu ya juu ya sekondari kati ya 2002 na 2004.

Kuanzia 2006 hadi 2009 alisoma Shahada ya Uhusiano wa Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Lincoln, Uingereza.

Baadaye alipata Stashahada ya Juu ya Usimamizi kutoka Institute of Administrative Management. Wasifu wa Bunge pia unaorodhesha masomo ya uzamili katika Chuo Kikuu cha Cumbria kuanzia 2019.

### Kusaka maisha

Kabla ya kuingia katika uongozi wa siasa, Deogratius alijenga uzoefu wa biashara na mawasiliano. Mwaka 2012 alikuwa meneja wa Kampuni ya matangazo ya A1 Outdoor; baadaye Mkuu wa Mauzo wa Smile Communications kati ya 2012 na 2014, Meneja wa Kanda wa Kampuni ya Tigo mwaka 2014 hadi 2015, na Mkuu wa Masoko wa GSM Group mwaka 2016.

### Kuingia siasa

Kama ilivyokuwa kwa Pancras Ndejembi - babu yake, Deogratius alipenda siasa kutoka kwake na inaelezwa babu yake alipenda kumuita "Mbunge" akimtania kwa kuwa alipenda kuhoji maswali mengi.



Deogratius Ndejembi akila kiapo kuwa Makamu wa Rais

Julai 2016, Rais John Magufuli alimteua kuwa Mkuu wa Wilaya ya Kongwa, akahudumu hadi 2020. Mwaka huo alichaguliwa kuwa Mbunge wa Chamwino kupitia CCM.

Baadaye aliteuliwa Naibu Waziri katika Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kisha akahamishiwa Tamisemi.

Machi 2024 alipandishwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, akisimamia kazi, vijana, ajira na watu wenye ulemavu. Julai mwaka huo akateuliwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

Baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2025, Rais Samia Suluhu Hassan alimteua kuwa Waziri wa Nishati, nafasi iliyomweka katikati ya miradi mikubwa ya uzalishaji na usafirishaji umeme.

Agosti 26, 2026, CCM ilimpendekeza kujaza nafasi iliyoachwa na Dkt. Emmanuel Nchimbi. Siku mbili baadaye, wabunge wote 324 waliopiga kura walimthibitisha; Agosti 29 akaapishwa Ikulu ya Chamwino, Dodoma, kuwa Makamu wa Rais wa 13 wa Tanzania.

Historia yake, kwa hiyo, ina sura mbili. Ni mrithi wa ukoo wenye alama nzito katika siasa za CCM Dodoma, lakini pia ni mtu aliyejenga uzoefu wake katika biashara, utawala na wizara tofauti. Babu yake alimwachia jina na mazingira ya kisiasa; nafasi ya Makamu wa Rais sasa itapima uwezo wa Ndejembi kujenga urithi wake mwenyewe.

Scanned with MOBILE SCANNER

Habari

# Utata alipo Dkt Nchimbi




*Aliyekuwa Makamu wa Rais Dkt. Emmanuel Nchimbi*

Na Waandishi WETU

NANI anajua alipo Dkt. Emmanuel Nchimbi, Makamu wa Rais wa Tanzania aliyetangaza kujiuzulu na kuachana na siasa na utumishi wa umma?

Ni swali lililoanza kusikika miongoni mwa Watanzania kupitia mitandao ya kijamii, mazungumzo ya wazi kwenye mijadala ya wasomi, wana harakati na hata "vijiweni."

Swali hili limegubikwa na kivuli na utata wa kiini hasa cha kujiuzulu kwa kiongozi huyo namba mbili nchini.

Dkt. Nchimbi ameshikilia wadhifa huo kwa kipindi cha chini ya miezi kumi, baada ya kuapishwa Novemba 3, 2025, akichukua nafasi ya Dkt. Philip Mpango, ambaye naye aliomba kupumzika kabla ya muda wake kwa sababu za kiafya.

Mara ya mwisho Dkt. Nchimbi kuonekana hadharani ilikuwa Agosti 22, 2026 kwenye ufunguzi wa mradi wa umeme wa maji wa Julius Nyerere (JNHP) wilayani Rufiji Mkoa wa Pwani.

Kwenye shuguli hiyo, kiongozi huyo alifanya kazi ya kumkaribisha Rais Samia Suluhu Hassan, na licha ya kupewa dakika 10 za kuzungumza, aliamua kutumia chini ya dakika moja kumkaribisha rais ambaye ndiye alikuwa mgeni rasmi.

Mawasiliano mengine ya Dkt. Nchimbi na Watanzania ni Agosti 25, 2026 kupitia akaunti yake ya Instagram ambako alipitisha barua yake fupi ya kutangaza kujiuzulu kwake nafasi ya makamu wa rais na siku iliyofuata, yaani Agosti 26, 2026 Chama Cha Mapinduzi (CCM) kikamfutia uanachama.

Hata hivyo, imebainika kuwa akaunti hiyo ya kijamii aliyoitumia kuujulisha umma kujiuzulu kwake ilikuwa hajaitumia tangu mwaka 2023.

Hili lilisababisha utata juu ya usahihi na uhalali wa barua hiyo ya kujiuzulu kutokana na kutokuwa hewani kwa muda mrefu.

Taarifa za kina zinaeleza kuwa mpaka sasa Dkt. Nchimbi hajulikani alipo, na hata mawasiliano yake ya simu ya kiganjani hayapatikani. Pambazuko lilijaribu kupiga simu ya mkononi ya Dkt. Nchimbi ambayo huitumia siku zote bila mafanikio.

Agosti 27, 2026 mmoja wa wasaidizi wake binafsi, alipoulizwa na Pambazuko kama amewasiliana na bosi wake, alikana kuwa msaidizi wake, lakini aliahidi kutoa namba ya msaidizi wa Dkt Nchimbi. Hata hivyo, tangu wakati huo hadi sasa hajawahi kutuma mawasiliano hayo.

Aidha, Waziri mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, akiwa kwenye kongamano lililoandaliwa na Kituo cha Demokrasia (TCD), Agosti 28, 2026 alisema tangu Dkt. Nchimbi alipoandika barua ya kujiuzulu Agosti 25, 2026 amekuwa akimtafuta kwenye simu bila mafanikio.

Katika kongamano hilo, Jaji Warioba, ambaye aliongoza tume ya kukusanyua maoni ya Katiba Mpya, alisema aliwasiliana na Dkt. Nchimbi baada ya kuona taarifa ya kujiuzulu kwake mitandaoni, na alipompigia simu kumuuliza, alimthibitishia kuwa ni kweli.

"Nilipoona kwenye mtandao kuna barua ya Nchimbi, binti yangu akaja, akasema Nchimbi ameandika barua ya kujiuzulu, nikakataa..."

Inaendelea Uk. 9

Scanned with MOBILE SCANNER

# Utata alipo Dkt Nchimbi

Inatoka Uk. 8

"Binti yangu mwingine akaja akasema ni kweli, ndipo nikampigia simu Nchimbi. Nikamuuliza kuna barua ina trend, nikamuuliza je, ni kweli umeandika barua ya ku-resign (kujiuzulu)? akasema ni kweli mzee, nikamuuliza, rais reaction yake ni nini (amepokeaje)? akasema bado... nikasema basi tutazungumza kwa urefu zaidi nijue kwa nini ume-resign..."

"Siku ya pili nikasikia halmashauri kuu inakutana, nikampigia, simu haikupokelewa… basi nikajua kwa kuwa bado ni makamu basi anaweza kuwa kwenye vikao vya Halmashauri Kuu..."

"Jioni likatoka tangazo kuwa kuna press conference ya CCM, nikampigia simu tena, lakini haikupokelewa, nikapeleka ujumbe, haukujibiwa. Kwa kawaida nikiandika alikuwa ana respond (anajibu) mapema tu..."

"Baadaye nikaona yaliyosemwa kwenye press conference, nikajaribu tena kupiga simu.. haikupokelewa..."

"Baada ya kuona tamko la Katibu Mkuu wa CCM kwamba chama kimemfukuza uanachama, nilimtafuta tena Dkt. Nchimbi lakini simu haipokelewi,"amesema Jaji Warioba.



*Aliyekuwa Makamu wa Rais Dkt. Emmanuel Nchimbi akiwa na Jaji Joseph Warioba wakati alipomtembelea nyumbani kwake.*

Jaji Warioba akaongeza; "Ndiyo nikaona wanasema amenyang'anywa simu zake. Sasa mimi inanishangaza kidogo maana nilikuwa kwenye chama, tulikuwa tunachukua hatua za nidhamu kwa utulivu, sasa waliponiambia sijui yuko kizuizini, bado sijaamini kwa kuwa sioni msingi yake..."

"Moja ya matatizo tuliyo nayo, ukiangalia ahadi zetu wana CCM, moja inasema nitasema kweli daima, fitina… mwiko, ipo kwenye ahadi zetu, lakini siku hizi ukisema ukweli, unazushiwa fitina."

Aidha, Jaji Warioba, ambaye amewahi kuwa Waziri Mkuu wa Tanzania katika serikali iliyoongozwa na Mwalimu Nyerere, anasema anaona kuna tatizo linalokwamisha kupatikana Katiba Mpya licha ya CCM kuahidi suala hilo kwenye ilani yake ya uchaguzi mwaka 2025.

Anasema anaona kilichofanya CCM imwadhibu Dkt. Nchimbi ni hatua yake ya kuwaambia Watanzania wapambanie Katiba Mpya.

"Katika tuhuma ambazo amepewa ni kusema hilo, na hiyo ndiyo inanipa wasiwasi, kweli tuna utashi wa siasa, ama tunataka tuendee hivi tusahau. Tutafika mwaka 2030 bila Katiba Mpya inayotumika. Na hali ninavyoiona kunaweza kuwa na mlipuko," ameonya Warioba.

Kauli tata za Nchimbi

Julai 24, 2026 katika mkutano mkuu wa 15 wa Mtandao wa Watetezi wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC) Dkt. Nchimbi aliwataka watanzania wapambane kuipata Katiba Mpya.

Kauli hii ilizua utata, huku baadhi ya watu wakihoji wananchi wapambane na nani iwapo iwapo serikali na CCM wote wanaitaka katiba hiyo mpya.

**Ziara kwa wastaafu**

Katika wiki za karibuni, Dkt. Emmanuel Nchimbi alikwenda kumtembelea Jaji Warioba, na siku chache baadaye alikwenda nyumbani kwa rais mstaafu, Jakaya Mrisho Kikwete. Hata hivyo haijulikana wazi juu ya uzito wa kile walichokizungumza.

Scanned with MOBILE SCANNER

Tafakuri ya Bagonza



Na Dkt. Benson BAGONZA

# Ukakasi na uhaini mamboleo




*Rais Samia Suluhu Hassan akishuhudia Deogratius John Ndejembi akiapishwa na Jaji Mkuu wa Tanzania, George Mcheche Masaju, kuwa Makamu wa Rais katika hafla iliyofanyika Ikulu ya Chamwino, mkoani Dodoma, Agosti 29, 2026.*



*Rais Samia Suluhu Hassan akiwa na Dkt. Emmanuel Nchimbi wakati wa Tamasha la Kizimkazi hivi karibuni.*

KAMA ilivyo na ukakasi kuzoea kumuita rais "mama au baba," inaweza kuwa na ukakasi kumwita makamu war ais; "mtoto au mwanetu."

Rais ni rais bila kujali jinsi yake. Makamu ni makamu bila kujali umri wake. Katika umri wa miaka 38, Nilikataa kuitwa "askofu mtoto" ili watu wasitumie utoto wangu kulihujumu kanisa.

Nakubali, hakuna shule ya urais au umakamu, lakini pia nchi siyo ya kufanyia mazoezi ya kuongoza. Nimewasikia watu kadhaa wakiwabeza wapinzani kuwa hawana uzoefu na kwamba nchi siyo ya kufanyia majaribio.

Uteuzi wa Makamu wa Rais wa Tanzania, Deo Ndejembi umemaliza kijembe hicho. Mtu yeyote, kijana, mzoefu, mpinzani, msomi, asiyesoma, anaweza kuongoza akiwa na utashi.

Namtakia Ndejembi kila jema. Amebeba dhamana kubwa katikati ya miiba. Asiuone ujana kama mtaji. Auone Umakamu kuwa mtaji.

Kinachosumbua vichwa vya wengi siyo umri wala makolokocho mengine. Ni namna ya kuingia na kutoka. Mtindo huweka kanuni isiyoandikwa.

Tumelazimishwa kulizoea neno "uhaini." Sasa tuna uhaini mamboleo. Uhaini una sura nyingi. Kuna haja ya kuliangalia hili neno kikatiba. Upo uhaini dhidi ya serikali. Upo pia uhaini dhidi ya wananchi.

Siyo wakati wote uhaini dhidi ya serikali ni uhaini dhidi ya wananchi. Siyo wakati wote uhaini dhidi ya wananchi ni uhaini dhidi ya serikali.

Upo uwezekano wa serikali na wananchi kutokuwa kitu kimoja na hivyo kuwezekana kufanyiana uhaini. Tumewalazimisha wananchi wengi waonekane ni wapinzani.

Ufa kati ya matajiri na maskini ni mkubwa sana. Ufa kati ya wananchi na serikali ni mkubwa mno. Haya mawili yanadai uongozi siyo utawala. Siyowakati wote, mtawala anakuwa ni kiongozi.

Nakusihi msomaji usijifanye kuwa Mjaluo. Tafakari kabla hujanifanya kuwa mhaini. Jipe muda ili nisikuone wewe ni mhaini dhidi yangu.

***Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.***

Scanned with MOBILE SCANNER



Na Dkt. Hellen Kijo BISIMBA

Kona ya Dkt. Bisimba

# Maswali mengi kujiuzulu Nchimbi, kuvuliwa uanachama

KATIKA siasa kuna matukio mengi ambayo ni vigumu kuyatabiri. Tukio moja huweza kutokea na maswali yakijitokeza jibu lake likawa rahisi.

Lakini wakati mwingine tukio hilo hilo likaweza kuzaa maswali ambayo majibu yake ni vigumu kupatikana.

Kujiuzulu kwa aliyekuwa Makamu wa Rais, Dkt. Emmanuel Nchimbi, kumeibua maswali mengi ambayo majibu yake ni vigumu kuyapata haraka.

Jumane ya Agosti 25, 2026 ambayo ilikuwa sikukuu ya Maulid, Watanzania tulipokea taarifa kwamba Dkt. Nchimbi amejiuzulu nafasi ya Makamu wa Rais na ameamua kustaafu siasa na utumishi wa umma, kuanzia Septemba 4, 2026 ambazo ni siku kama kumi baada ya taarifa.



Katika taarifa yake, alisema amefikia uamuzi huo baada ya kuridhika kwamba Rais Samia Suluhu Hassan anatamani mabadiliko katika nafasi hiyo. Mara Rais naye akatangaza kukubali kujiuzulu kwake.

Lakini kabla Watanzania hawajapata muda wa kutafakari maana ya kujiuzulu huko, likatokea jambo jingine kubwa zaidi; yaani, chama chake CCM kikaitisha vikao na kumfukuza Dkt. Nchimbi uanachama.

Kwa mujibu wa Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Asha-Rose Migiro, vikao vya Kamati Kuu na Halmashauri Kuu vilijadili suala la nidhamu na maadili na kubaini kuwa Katiba, Kanuni na taratibu za chama zilikuwa zimekiukwa.

Hata hivyo, maelezo ya kina kuhusu kosa hilo hayajawekwa wazi kwa umma. Hapa ndipo ninapojiuliza; kulikoni?

Ikiwa Dkt. Nchimbi aliamua kujiuzulu kwa sababu alitambua kuwa rais anataka mabadiliko, kwa nini ndani ya muda mfupi namna hiyo afukuzwe na chama chake?

Je, kujiuzulu kulikuwa uamuzi wake mwenyewe, au kulikuwa na jambo jingine nyuma yake ambalo Watanzania hatujaambiwa?

Na kama kulikuwa na suala la nidhamu na maadili, ni muhimu kwa umma kuelewa; ni kosa gani hasa lililofanyika? Siyo kwa nia ya kumhukumu Dkt. Nchimbi, bali kwa sababu alikuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyepitia katika uchaguzi mkuu na hadi akitangaza kujiuzulu alikuwa mmoja wa viongozi wakuu wa nchi.

Jambo jingine linalostahili kutafakariwa ni kasi ya matukio. Kujiuzulu kwa Makamu wa Rais, kufukuzwa kwake CCM na kupitishwa kwa jina la mrithi wake, aliyekuwa Waziri wa Nishati, Dkt. Deogratius Ndejembi, vimetokea kwa kasi kubwa sana.

CCM imempendekeza Ndejembi kwa nafasi hiyo na tayari ameapishwa rasmi juzi.

Kwa jicho la kawaida huoni kabisa hiyo kasi ilitokea kwa sababu zipi zaidi ya kudhani ilikuwepo katika mlolongo wa matukio kwa ndani na yalipojitokeza watazamaji ndiyo tunashangaa.

Hii haimaanishi kwamba tunakosoa uteuzi wa mrithi. Kasi ndiyo imezua swali la msingi liendelee kusikika; Je, haya yalikuwa yamepangwa tayari, au yalitokana na matukio yaliyotokea ghafla?

Dkt. Nchimbi aliwahi kuwa Katibu Mkuu wa CCM kabla ya kuwa mgombea mwenza wa Rais Samia katika uchaguzi wa 2025.

Amekaa katika nafasi ya Makamu wa Rais kwa siku 295 tu. Kwa hiyo, kuondoka kwake si jambo dogo.

Ni tukio linalostahili maelezo ya kutosha, hasa kwa kuwa limefuatiwa na hatua kali ya kufukuzwa chama.

Chama kilijua ana hatia za kimaadili kikasubiri atangaze kujiuzulu ndiyo kiamue kumfukuza au kujiuzulu ndilo kosa la kimaadili?

Ingefaa tukajua kulikoni. Katika demokrasia, siyo lazima wananchi waambiwe kila jambo la ndani ya hicho chama.

***Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337240.***

Scanned with MOBILE SCANNER

# Lissu alivyohitimisha mchuano wa ushahidi mahakamani



Na Mwandishi WETU

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na maendeleo (Chadema), Tundu Lissu, amehitimisha safari ya siku tano ya kuwasilisha ushahidi wake binafsi, katika kesi ya uhaini inayomkabili.

Lissu anayekabiliwa na kesi ya uhaini namba 19605/2025 alianza utetezi wake Ijumaa - Agosti 21, 2026, ikiwa ni mwendelezo wa kesi hiyo iliyodumu kwa zaidi ya mwaka mmoja sasa.

Katika uamuzi wa mahakama baada ya kusikiliza ushahidi wa upande wa mashtaka, jopo la majaji watatu wanaosikiliza kesi hiyo wakiongozwa na Jaji Jaji Dunstan Ndunguru, liliamua Lissu ana kesi ya kujibu, hatua iliyofungua njia kwa mwanasiasa huyo kuanza kujitetea. Majaji wengine ni James Karayemaha na Ferdinand Kiwonde.

Ijumaa iliyopita, ikiwa ni wiki moja tangu alipoanza kutoa ushahidi wake, Lissu alimaliza kwa mvutano wa kimantiki, akipambana na mawakili wa serikali ambao walitaka asipate nafasi ya kuhojiwa tena ili kusahihisha maeneo aliyoona yalikuwa na mapungufu baada ya maswali ya dodoso kutoka kwao.

Kabla ya kuhitimisha ushahidi wake ili kuruhusu kuanza kusikilizwa kwa mashahidi wengine, Lissu aliibua mabishano makali baada ya kutaka ahojiwe tena ili atoe ufafanuzi katika baadhi ya maeneo.

Ombi hilo lilipingwa vikali na kiongozi wa jopo la mawakili wa serikali, Nassor Katuga, ambaye aliieleza mahakama kuwa upande wa Jamhuri unafahamu kuhojiwa tena ni njia moja wapo ya shahidi kutoa ushahidi na ipo kisheria na ila waliomba kwa mujibu wa sheria shahidi ajikite kwenye yale maswali aliyohojiwa na asilete jambo jipya.

"Ni jinsi gani atajihoji ili kufikia lengo la kutoa ufafanuzi wa majibu yake wakati wa kuhojiwa na upande wa pili, suala ambalo tunaomba mahakama hii tuulize, shahidi ni mtu ambaye anajiwakilisha mwenyewe sasa kuhojiwa tena itafanyikaje?

"Ajiulize maswali mwenyewe na ajijibu mwenyewe kuna hatari ya kuleta ushahidi mpya kabisa maana lengo la kuhojiwa tena ni kufafanua sasa kujiuliza mwenyewe atakuwa hakimu wa mwenendo wake mwenyewe, sasa zile kanuni zetu zinakinzana na hiki…"

"Kama angekuwa na wakili sawa ila wewe mwenyewe ujiulize na ufafanue ili kuepuka mkanganyiko mahakama inaweza ikamuuliza kwa vile vipande ambavyo inaona vinahitaji ufafanuzi," alisema Katuga.

Katuga aliwaeleza majaji katika kesi hiyo kuwa wanataka mahakama imuelekeze shahidi atoe maelezo kama itahitajika kufanya hivyo kwenye majibu yake yenye maana zaidi ya moja na siyo kufungua sababu ya kutoa uwanda wa kutoka nje ya yale ambayo yanayohitaji ufafanuzi.

Inaendelea Uk. 13

Scanned with MOBILE SCANNER

# Lissu alivyohitimisha

Inatoka Uk. 12

Baada ya ombi hilo la Katuga, Lissu aliieleza mahakama kuwa kwa kuwa ni mwongozo, suala la kuhojiwa tena ni haki ya shahidi aliyekuwa akihojiwa na upande wa pili, ndio maana kwa mujibu wa sheria, shahidi atakuwa wa kwanza kutoa ushahidi na kama upande wa pili utamhoji na shahidi huyo akitaka kuhojiwa tena ni haki yake na kama ni haki alipaswa kunyamaza kimya.

"Wakili wa serikali mkuu anasema atajiongozaje sababu hana wakili, ukweli kwamba shahidi ndiye mshitakiwa na anajiwakilisha mwenyewe kitakachofanyika ni kurejea maswali yaliyoulizwa na majibu yake na kufafanua kwa hiyo hakuna chochote cha kutolea mwongozo sheria iko wapi, hii inaweza kuwa ni fursa ya kuingiza mambo mapya?

"Utaratibu uko wazi kama kutakuwa na mambo mapya watafanya pingamizi kwa hiyo hawapaswi kuwa na hofu ya bure sasa waheshimiwa majaji hamna mwongozo wa kutoa," alisema Lissu.

Maelezo hayo ya Lissu yalikubaliwa na jaji ambaye alisema huo ndio mwongozo wenyewe, hatua iliyomfanya Lissu kuwaomba majaji kuwa wawe makini kwa kuwa iwapo watalazimika kutoa mwongozo kwenye jambo dogo kama hilo, inabidi wawe macho na upande wa mashtaka.

Baada ya muongozi huo wa jaji, Lissu aliendelea kutoa ufafanuzi katika baadhi ya maeneo aliyoona anahitaji kufanya hivyo, akiendelea kulizwa maswali ya dodoso na mawakili wa serikali kila walipoona wanahitaji kufanya hivyo.

Lissu alitumia nafasi hiyo kutoa ufafanuzi wake katika kila eneo aliloona lina upungufu au alitoa majibu ambayo hayakueleweka vizuri wakati alipokuwa akitoa maelezo au kuulizwa maswali ya dodoso na mawakili wa Serikali.

#### Alivyojitetea

Katika siku tano za kutoa ushahidi wake, Lissu aliieleza mahakama kwa urefu kuhusu maisha yake, ikiwemo namna alivyoshiriki katika harakati za kutetea haki za watu katika maeneo mengi nchini tangu alipokuwa shule.

Lissu alitumia nafasi hiyo kueleza pia safari yake ya kiaisa na misukosuko aliyoipata ikiwemo kukamatwa, kufunguliwa kesi kila mara na hata namna alivyonusurika kuuawa wakati akiwa mbunge, baada ya watu wasiojulikana kumvamia alipokuwa katika eneo la makazi yake mjini Dodoma mwaka Septemba 2017.

Pia alieleza safari yake ya matibabu nje ya nchi na hatimaye kujikuta akiishi uhamishoni, hadi alipokutana na Rais Samia Suluhu Hassan, alivyorejea nchini na kushiriki kwenye uchaguzi mkuu wa 2020 akiwa mgombea dhidi ya John Magufuli.

Lissu pia alieleza mazungumzo waliyofanya na Rais Samia mwaka 2021 akwia nchini Ubelgiji hadi yeye na wenzake waliokuwa nje ya nchi kwa kuhofia usalama wao walipoamua kurejea nchini.

Katika kesi hiyo, Lissu aliieleza mahakama kuwa yeye atajitetea mwenyewe na alianza kwa kutoa utetezi wake huku akiwataja mashahidi wake wengine kuwa ni kiongozi mkuu wa Serikali, Rais Samia Suluhu Hassan, aliyekuwa Makamu wa Rais, Dkt. Phillip Mpango, aliyekuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Jenerali Jacob Mkunda.

Wengine ni Inspekta wa jeshi la Polisi (IGP) Camillus Wambura, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) Ramadhani Kingai, Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Suleiman Mombo na Kamishna wa Polisi (DCP) Ramadhani Ng'anzi.

Pia aliwataja wanaharakati kutoka nchi za Afrika Mashariki ambao ni Agather Atuhaire, Boniface Mwangi, Dkt Willy Mutunga, Martha Karua, mwandishi wa habari John Marwa, na viongozi wa Chadema ambao ni Amani Golugwa, John Heche na John Mnyika.

Baada ya Lissu kuhitimisha kutoa ushahidi wake, mahakama ilianza kusikiliza ushahidi wa mashahidi wengine wa upande wa utetezi kwa kufanya mahojiano na Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika mahakamani hapo ambaye ataendelea kutoa ushidi wake leo, Jumatatu Agosti 31, 2026.

Scanned with MOBILE SCANNER

■ Habari

# El-Nino yashtua serikali, mikakati yaanza kukabili



*Wafanyabiashara wa Mbezi wakivunja vibanda vyao vilivyokuwa juu ya mitaro ya kupitisha maji ya mvua ikiwa ni maandalizi ya kukabiliana na mvua za El Nino zinazotarajia kunyesha kuanzia mwezi ujao. (Picha na Pambazuko).*

Na Mwandishi WETU

MIKAKATI ya kukabiliana na athari zinaoweza kujitokeza kutokana na mvua za El-Nino imeshika kasi, huku serikali ikisisitiza wakuu wa mikoa, taasisi za umma, binafsi na wananchi kuhakikisha wanaandaa mazingira ya kupunguza athari zinazotokana na mvua hizo.

Hatua hizo zinakuja siku chache baada ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) kutoa tahadhari ya uwezekano wa kutokea kwa mvua za El Niño katika mikoa 14 nchini kuanzia mwishoni mwa Septemba hadi Desemba mwaka huu, zitakazotokana na mvua za vuli.

Tayari tahadhari nyingine imetolewa na Umoja wa Ulaya (EU) kuhusu hali ya mabadiliko ya tabianchi, ikieleza kuwa taarifa hiyo inaeleza kuwa bahari duniani zimefikia viwango vya juu zaidi vya joto kuwahi kurekodiwa, huku hali hiyo ikihusishwa na athari za mabadiliko ya tabianchi yanayosababishwa na shughuli za binadamu.

Katika kukabiliana na hali hiyo, Agosti 22, Rais Samia Suluhu Hassan, aliwataka wakuu wa mikoa, wilaya na taasisi za serikali kujiandaa mapema kukabiliana na mvua kubwa zinazotabiriwa nchini, ili kuepusha maafa na madhara kwa wananchi.

"Niwaombe nendeni mkajitayarishe, mkaweke mazingira sawa ili mvua hizo zitakapoanza zisilete maafa makubwa kwa wananchi wetu," alisema.

Alisema tahadhari ambazo TMA imeanza kutoa zinapaswa kuchukuliwa kwa uzito na viongozi kuhakikisha mazingira yanaandaliwa ili kupunguza athari zinazoweza kusababishwa na mvua hizo.

"Kwa hiyo niwaombe sana, tahadhari zimeanza kutolewa, hatua zichukuliwe ili mvua hizi zisilete madhara kwa wananchi wetu," alisema Rais Samia.

Alitoa kauli hiyo wakati akizungumza na wananchi mkoani Pwani mara baada ya kuzindua mradi wa kuzalisha umeme wa megawati 2,115 wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere (JHPP).

Tahadhari hizo za serikali zikaendelea kupitia Waziri Mkuu, Mwigulu Nchemba, kueleza bungeni Alhamisi Agosti 27, 2026 kuwa Serikali imejipanga kukabiliana na athari zinaoweza kujitokeza kutokana na mvua hizo za El-Nino.

Dkt. Nchemba aliwahakikishia wabunge kuwa serikali imejipanga vyema kuhakikisha kwamba maeneo yatakayoathirika yanapatiwa misaada ya haraka.

"Bunge lilipitisha mabadiliko ya sheria kwenye sheria ya fedha yanayoelekeza fedha kwenda moja kwa moja kwenye mifuko ya barabara na mingine…"

"Nawapongeza Wizara ya Fedha na TRA kwa kuanza kuzipeleka fedha hizo ambazo ni zaidi ya shilingi bilioni 320 na kuiwezesha mifuko kukabiliana na mambo kama haya," alisema.

Alielekeza Wakala wa Barababara Tanzania (Tanroads) na Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura) kupitia maeneo yote korofi yanayoweza kufanya mrundikano wa maji na kuleta mafuriko na kuhakikisha yanatengenezewa mifereji.

Inaendelea Uk. 15

Scanned with MOBILE SCANNER

# El-Nino yashtua...

Inatoka Uk. 14

Alitoa rai kwa Watanzania wote kuwa na tahadhari na jambo hili ambalo limeshatolewa taarifa na kila Mtanzania kufanya tathmini ya pale anapoishi kwa kuangalia mazingira yao kwa kuwa wanajua historia ya mikondo ya katika maeneo wanayoishi.

Kwa upande wake, Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, amewataka wananchi kutunza sehemu ya chakula walichovuna mwaka huu, kwani mvua hizo za El Niño zinaqweza kuathiri mazao mashambani au kwenye maghala.

Silinde alitoa mwito huo Agosti 26, 2026, wakati wa kipindi cha maswali na majibu katika mkutano wa Nne wa Bunge la 13 wakati akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalumu kupitia CCM Mkoa wa Iringa, Nancy Nyalusi, aliyetaka kujua Serikali itaanza lini kununua mahindi ya wakulima.

Silinde alisema Waziri wa Kilimo, Daniel Chongolo, tayari ameelekeza mamlaka ya mazao mchanganyiko kuanza ununuzi wa mazao, huku Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) ukitarajiwa kuongeza nguvu katika ununuzi haraka.

Akizungumzia tahadhari za hali ya hewa, Silinde alisema utabiri unaonyesha uwezekano wa mvua nyingi katika baadhi ya maeneo ya Afrika Mashariki kutokana na kuimarika kwa El-Niño.

Aliwataka wananchi kuepuka kuuza chakula chote baada ya mavuno, akisema tabia hiyo imekuwa ikiwafanya baadhi yao kukumbwa na upungufu wa chakula baadaye na kulazimika kutegemea msaada.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Amos Makala, amezielekeza kamati za usalama mkoa na wilaya za Karatu na Ngorongoro, pamoja na timu ya menejimenti ya Mamlaka ya Hifadhi Ngorongoro (NCAA), kuweka mikakati ya kukabiliana na mvua za El-Nino.

Katika kikao kilichofanyika kwenye ukumbi wa Mikutano Makao makuu ya NCAA wilaya ya Karatu Agosti 26, 2026, Makala alizikumbusha kamati za maafa katika kila wilaya zikutane na kuweka mikakati ya kukabiliana na mvua hizo kama ambavyo Rais Samia ameelekeza.

Agosti 18, 2026 TMA ilitoa angalizo kuhusu uwezekano wa kuwepo kwa mvua kubwa zinazohusishwa na hali ya hewa ya EI Niño yenye nguvu kuanzia Septemba na hadi Desemba 2026, huku athari zake zikitarajiwa kuendelea hadi mwanzoni mwa mwaka 2027.

Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Ladislaus Chang'a, alisema El Niño yenye nguvu inaweza kusababisha vipindi vya mvua kubwa pamoja na kuanza mapema kwa mvua za msimu katika baadhi ya maeneo.

Chang'a alizitaka Idara na taasisi nchini, ikiwemo Mamlaka za Bandari, reli, usafiri wa anga pamoja na sekta ya afya, kuchukua tahadhari na kujiandaa mapema kukabiliana na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na mvua hizo.

El-Nino inatarajiwa katika ukanda huu wa Afrika Mashariki, ambapo wanasayansi wana wasiwasi kuhusu El-Nino ya mwaka huu kwa sababu mbili moja ikiwa ni ukubwa wake.

El-Nino iliyowahi kuwa mbaya zaidi ni ile ya mwaka 1998, na Umoja wa Mataifa umeonya, hali ambayo itaongeza joto katika sayari ambayo tayari inakabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabianchi. Shirika la Hali ya Hewa Duniani (WMO) limesema El-Niño hii huenda ikatokea mwaka 2026, na kusababisha hali mbaya zaidi za hewa katika sehemu kubwa za dunia. Utabiri kadhaa kutoka mashirika ya kitaifa ya hali ya hewa unaonyesha huenda ikawa mojawapo ya El-Niño zenye nguvu zaidi kuwahi kurekodiwa — kinachoweza kuitwa 'super' El-Niño."



*Mitaro ya kupitisha maji mvua iliyokuwa imefunikwa na vibanda vya wafanyabiashara eneo la Mbezi ikiwa wazi baada ya vibanda hivyo kusogezwa pembeni ikiwa ni maandalizi ya kukabiliana na mvua za El Nino zinazotarajia kunyesha kuanzia mwezi ujao. (Picha na Pambazuko).*

Scanned with MOBILE SCANNER

Habari

# OMO awapa wawakilishi jukumu zito

Na Mwandishi WETU, Dunga

MWENYEKITI wa ACT Wazalendo, Othman Masoud Othman, almaarufu OMO, amewataka wajumbe wa wawakilishi kutoka chama hicho kutumia nafasi zao kujenga taasisi imara za uwajibikaji.

Pia, amewahimiza kuhakikisha maridhiano yaliyofikiwa kati ya chama hicho na CCM yanazaa mabadiliko yanayogusa maisha ya Wazanzibari.

Othman amesema mafanikio ya maridhiano hayo hayatapimwa kwa makubaliano yaliyosainiwa pekee, bali kwa uwezo wa viongozi na taasisi za serikali kubadili mfumo wa uendeshaji wa nchi na kuleta matokeo ya kiuchumi na kijamii.

Ametoa kauli hiyo huko Dunga, Wilaya ya Kati, Unguja, alipokutana na viongozi wa ACT Wazalendo kutoka majimbo matatu ya mkoa huo kwa ajili ya kutoa ufafanuzi kuhusu yaliyomo katika makubaliano yaliyofikiwa kati ya ACT Wazalendo na CCM na kusainiwa Julai 9, 2026, Ikulu Zanzibar.

Akizungumza mbele ya viongozi hao, Othman amesema Zanzibar haiwezi kujenga uchumi wenye ushindani wala kuharakisha maendeleo bila kuwa na viongozi na watendaji wenye uwezo, uadilifu, umakini na utayari wa kuwajibika.

Amesema uzoefu wa mataifa yaliyofanikiwa, ikiwemo Singapore, unaonyesha kuwa rasilimali pekee hazitoshi kujenga uchumi imara bila kuwa na mifumo mizuri ya utawala na watu wenye uwezo wa kuisimamia.

"Kiongozi anayetaka kujenga nchi hatizami uchaguzi; anaangalia hatma na mustakabali wa nchi. Anaangalia namna ya kuijenga nchi, hasa anapoona mwelekeo uliopo siyo mzuri na unaelekea kuwa mbaya zaidi," amesema.



Kauli hiyo inaweka uzito mpya kwenye nafasi ya wawakilishi katika kipindi ambacho Zanzibar inaingia katika hatua ya utekelezaji wa makubaliano ya kisiasa yaliyolenga kupunguza migawanyiko na kujenga mazingira mapya ya kisiasa.

### Wawakilishi na mabadiliko

Othman, ambaye ni Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar mstaafu, amesema moja ya maeneo muhimu katika utekelezaji wa maridhiano ni kujenga taasisi zinazoweza kuisimamia serikali na kuhakikisha viongozi wanawajibika kwa wananchi.

Amesema Baraza la Wawakilishi linapaswa kuwa miongoni mwa mihimili yenye uwezo wa kuihoji serikali na kufuatilia utekelezaji wa mipango ya maendeleo.

Kwa mtazamo huo, amesema ubora wa Baraza la Wawakilishi hauanzi siku linapokutana kufanya shughuli zake, bali huanzia katika mchakato wa kisheria unaomuwezesha mwakilishi wa wananchi kupata nafasi hiyo.

"Nidhamu kubwa ya kuendesha nchi ni kuhakikisha tuna watumishi na viongozi bora wenye uwezo wa kusukuma kasi ya ufanisi, sambamba na kuwa na vyombo madhubuti vya kuichunga serikali," amesema. Amesisitiza kwamba taaluma pekee haiwezi kuwa kipimo cha uongozi bora bila kuambatana na uadilifu.

### Uchumi bado ni changamoto

Katika sehemu nyingine ya hotuba yake, Othman amesema Zanzibar imefikia hali ngumu kiuchumi na kimaendeleo licha ya kuwa na rasilimali ambazo, kwa mtazamo wake, zingeweza kubadili maisha ya wananchi.

Amesema hali hiyo inahitaji viongozi kuangalia zaidi mustakabali wa nchi kuliko maslahi ya kisiasa ya muda mfupi.

OMO amesema mwelekeo huo ndio uliokuwa msingi wa mazungumzo kati ya ACT Wazalendo na CCM, akisisitiza kwamba dhamira kuu ilikuwa kujenga nchi.

Scanned with MOBILE SCANNER

# Laini moja ya simu kutumika nchi 190

Na Mwandishi WETU

WASAFIRI wanaokwenda nje ya Tanzania, sasa wataweza kupata huduma ya intaneti bila kubadilisha laini zao za simu au kununua kadi za simu wanapowasili, baada ya kuzinduliwa kwa jukwaa la Kwetu eSIM.

Huduma hiyo inayopatikana katika nchi 190 duniani inawawezesha watumiaji kununua vifurushi vya intaneti kabla ya kuanza safari na kuviwasha wanapowasili katika nchi wanayokwenda kupitia simu zinazotumia teknolojia ya eSIM.

Kwa majibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa iliyotolewa na Kampuni ya Kwetu eSIM, kupitia programu hiyo, mtumiaji anaweza kuchagua nchi anayokwenda, kununua kifurushi cha data na kukiwezesha kwa kutumia QR code au msimbo wa kuwezesha huduma hiyo, bila kulazimika kutoa Sim kadi iliyopo kwenye simu.

Imeeleza kuwa hatua hiyo inalenga kupunguza changamoto ambazo wasafiri hukutana nazo wanapokuwa nje ya nchi, ikiwamo gharama kubwa za huduma za roaming, usumbufu wa kutafuta kadi za simu simu za nchi husika na kulazimika kusubiri katika maduka ya huduma za mawasiliano baada ya kuwasili.

Taarifa hiyo imeeleza kuwa kuwa Kwetu eSIM pia inaruhusu malipo kwa kutumia kadi pamoja na huduma za fedha kwa mitandao yote ya simu huku maelezo yote yakiwa yanaoatikana kupitia tovuti ya kwetuesim.com au https://kwetuesim.com/sw/.

Imeeleza kuwa watumiaji pia wanaweza kuweka fedha kwenye pochi ya ndani ya programu hiyo kwa ajili ya kufanya malipo.

Huduma hiyo imeelezewa kuwa inaweza kutumiwa na wasafiri wa kibiashara, watalii, wanafunzi, watu wanaokwenda kutembelea familia nje ya nchi pamoja na kampuni zinazowapeleka wafanyakazi katika safari za kimataifa.

Miongoni mwa huduma zinazopatikana ni uwezo wa kuongeza kifurushi cha data mtumiaji anapokaribia kukimaliza akiwa nje ya nchi. Mtumiaji hahitaji kuondoa au kusakinisha upya eSIM yake ili kuongeza data.

Pia, mtumiaji anaweza kumnunulia mtu mwingine kifurushi kama zawadi. Kipengele hicho kinaweza kutumiwa na mtu anayemtayarishia ndugu, rafiki au mfanyakazi wake huduma ya mawasiliano kabla ya kusafiri.

Kwa mujibu wa maelezo katika taarifa yao, huduma hiyo inapatikana katika zaidi ya nchi 190 na inahudumia maeneo ya Afrika, Ulaya, Asia-Pacific, Amerika na Mashariki ya Kati.

Programu hiyo inapatikana katika mifumo ya iOS, Android na Huawei, huku ikisaidia lugha saba ambazo ni kiingereza, kiswahili, kifaransa, kihispania, kiitaliano, kiarabu na kichina.

Huduma hiyo pia inaonyesha matumizi ya data kupitia vipengele vinavyopatikana kwenye skrini ya simu, hatua inayomwezesha mtumiaji kufuatilia matumizi yake na kuongeza kifurushi anapohitaji.

"Uzinduzi wa Kwetu eSIM unakuja wakati matumizi ya simu janja na huduma za kidijitali yakiendelea kuongezeka, huku wasafiri wakihitaji njia rahisi ya kuendelea kutumia intaneti bila kutegemea huduma za roaming za waendeshaji wa simu wa nchi wanayotoka.

Kwetu eSIM imesema watumiaji wanaweza kupata huduma hiyo kupitia Apple App Store na Google Play, huku vifurushi pia vikipatikana kupitia tovuti ya kampuni.

Kampuni hiyo imeeleza kuwa lengo lake ni kuunganisha huduma za mawasiliano za kimataifa na njia za malipo zinazopatikana katika masoko ya ndani, ili kurahisisha upatikanaji wa intaneti kwa wasafiri.

Hata hivyo, upatikanaji na matumizi ya eSIM hutegemea kama simu ya mtumiaji inaunga mkono teknolojia hiyo pamoja na masharti ya mtandao katika nchi anayokwenda.

Scanned with MOBILE SCANNER

# Fitch yaipa Tanzania mtazamo chanya kiuchumi




Na Mwandishi WETU

KAMPUNI ya kimataifa ya Fitch Rating inayojihusisha kufanya tathmini ya uwezo wa nchi kukopesheka katika masoko ya fedha ya kimataifa, imetoa alama ya B+ kwa Tanzania katika tathmini yake ya hivi karibuni.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Fedha wiki iliyopita inasema kuwa hatua hiyo ya Fitch inadhihirisha kuimarika kwa misingi ya uchumi na uimara wa sera za uchumi jumla nchini.

Kwa mujibu wa ripoti ya kampuni hiyo iliyochapishwa katika tovuti yake rasmi, Fitch imesema mabadiliko hayo yanatokana na kuimarika kwa akiba ya fedha za kigeni, kuwepo kwa nakisi ya bajeti inayodhibitika na kuendelea kwa ukuaji wa uchumi.

Fitch inaeleza kuwa kwa pamoja mambo haya yanatarajiwa kuongeza mapato kusaidia kuhudumia bajeti ya nchi pamoja na kupunguza mzigo wa deni la serikali. Aidha, Fitch imesema akiba ya fedha za kigeni nchini inatarajiwa kuongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 6.3 mwishoni mwa mwaka 2025 hadi kufikia dola bilioni 7.9 mwaka 2028, sawa na uwezo wa kugharamia malipo ya nje kwa takribani miezi 3.3.

Fitch imeeleza kuwa kupungua kwa changamoto katika soko la fedha za kigeni na kuongezeka kwa unyumbufu wa kiwango cha ubadilishaji wa fedha, kumechangia kupunguza baadhi ya hatari za muda mfupi, huku akiba ya dhahabu iliyoko Benki Kuu, inayokadiriwa kufikia dola za Marekani bilioni 2.4, inaweza kuongeza zaidi kinga ya nchi dhidi ya mishtuko ya nje katika nyanja za uchumi.

Katika upande wa bajeti na usimamizi wa deni, Fitch imekadiria kuwa nakisi ya bajeti kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 2026 ilikuwa asilimia 2.8 ya Pato la Taifa, ikichangiwa na ongezeko la ukusanyaji wa mapato na athari ndogo za ruzuku za mafuta katika utekelezaji wa bajeti na inatarajiwa nakisi hiyo kubaki karibu asilimia 3 ya Pato la Taifa hadi mwaka wa fedha 2028.

Katika ripoti yake Fitch imebainisha pia kuwa mapato ya kodi yaliongezeka kutoka asilimia 14.6 hadi asilimia 15.6 ya Pato la Taifa kati ya 2023 na 2025.

Fitch pia imetabiri kuwa uwiano wa deni la serikali kwa Pato la Taifa utapungua kutoka asilimia 48.9 mwaka 2025 hadi asilimia 46.2 mwaka 2028, kiwango ambacho kitakuwa chini ya wastani wa asilimia 55 unaokadiriwa kwa nchi zilizo katika kundi la ukadiriaji wa B.

Imeeleza kuwa kupungua kwa deni kutachangiwa na ukuaji mkubwa wa Pato la Taifa kwa thamani ya sasa pamoja na kuwezesha kuwa na nakisi ndogo ya msingi ya bajeti.

Kwa upande mwingine Fitch imepongeza hatua zinazochukuliwa kuboresha usimamizi wa fedha za umma, ikibainisha kuwa hadi Machi 2026, kiasi cha madeni ya serikali yaliyothibitishwa kwa wazabuni na marejesho ya kodi kilikuwa kimepungua hadi asilimia 0.2 ya Pato la Taifa kutoka asilimia 1.2 ya Desemba 2022.

Inaendelea Uk. 19

Scanned with MOBILE SCANNER

# Fitch yaipa Tanzania

Inatoka Uk. 18

Kwa upande wa ukuaji wa uchumi, Fitch inatarajia Tanzania kuendelea kufanya vizuri ikilinganishwa na wastani wa nchi zilizo katika kundi la B, ikitabiri ukuaji wa Pato la Taifa kwa asilimia 5.8 mwaka 2026, dhidi ya wastani wa asilimia 3.7 kwa kundi hilo.

Fitch inakadiria kuwa uchumi utakua kwa wastani wa asilimia 6.1 katika kipindi cha 2027–2028, ukichochewa na uwekezaji wa umma, utalii, nafasi ya Tanzania kama kitovu cha usafirishaji na biashara kikanda pamoja na ukuaji wa sekta ya madini.

Wakati huohuo, Fitch inatarajia mfumuko wa bei wa wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2026, kutoka asilimia 3.3 mwaka 2025, lakini bado ukiwa chini ya wastani wa asilimia 5.6 unaotarajiwa kwa nchi za kundi la B.

Fitch imeeleza pia kuwa Tanzania imepiga hatua katika kuboresha mfumo wa sera za uchumi jumla tangu mwaka 2023, kupitia maboresho ya kitaasisi na kiutendaji yaliyoimarisha uhuru wa benki kuu, mfumo wa uendeshaji wa kiwango cha ubadilishaji wa fedha na usimamizi wa soko la fedha za kigeni.

Aidha, wameongeza kuwa maboresho hayo yanaweza kuongeza uwezo wa Tanzania kukabiliana na mishtuko ya kiuchumi, ingawa baadhi yake bado yanahitaji kuthibitishwa kupitia utekelezaji wake kwa muda.

Pia wasiwasi wa awali kuhusu uwezo wa takwimu za kitaifa kuakisi mabadiliko ya ukuaji wa uchumi umepungua baada ya kukamilika kwa zoezi la kubadili mwaka wa msingi wa Pato la Taifa Juni 2026.

Fitch inatazamia pia kuendelea kuimarika kwa akiba ya fedha za kigeni, kuongezeka kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato, udhibiti wa matumizi ya serikali na kushuka kwa uwiano wa deni kwa Pato la Taifa ni miongoni mwa mambo yatakayoweza kuchangia hatua zaidi ya kuboresha ukadiriaji wa Tanzania.

Shirika hilo limeeleza kuwa kuongezeka kwa imani kwamba maboresho ya mfumo wa sera za uchumi jumla yataendelea kuimarisha uwezo wa nchi kukabiliana na mishtuko ya nje na kudumisha utulivu wa uchumi kutakuwa msingi muhimu wa hatua hiyo.

Kwa ujumla, Fitch imeona mwenendo wa uchumi wa Tanzania ukiwa na msingi chanya, huku ikiweka mkazo katika kuendelezwa kwa nidhamu ya fedha, kuimarishwa kwa mapato ya ndani na utekelezaji endelevu wa maboresho ya sera ili kujenga mazingira imara zaidi ya uchumi.



*Muuguzi wa Hospitali ya Magomeni katika Manispaa ya Kinondoni, Sophia Mkama, akiwapatia chanjo ya polio wanafunzi walio chini ya miaka 10 wa Shule ya Msingi Ndugumbi iliyopo Mwembechai baada ya kampeni hiyo kuzinduliwa Jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na Pambazuko).*

Scanned with MOBILE SCANNER

## Uchambuzi

# Kuondoka Nchimbi kwafungua maswali magumu zaidi



*Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Makamu wa Rais Balozi, Dkt. Emmanuel Nchimbi na Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Balozi Dkt. Asha-Rose Migiro baada ya kuwasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Dar es Salaam akitokea Urusi. Juni 6, 2026.*

Na Ansbert Ngurumo

MATUKIO ya kujiuzulu na kufukuzwa kwa Dkt. Emmanuel Nchimbi yameacha gumzo kubwa kitaifa, na yameongeza sura katika kitabu cha uongozi wa nchi, hasa wanapojadiliwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano ya Tanzania tangu Abeid Karume hadi Deo Ndejembi.

Lakini historia haitamkumbuka Nchimbi kwa sababu tu alikuwa makamu wa rais aliyejiuzulu. Itamkumbuka zaidi kwa mazingira ya kuondoka kwake.

Alitangaza kujiuzulu Agosti 25, 2026, akisema angeondoka rasmi Septemba 4. Rais Samia Suluhu Hassan akakubali. Siku iliyofuata, kabla hata tarehe hiyo haijafika, CCM ikamfukuza uanachama kwa madai ya kukiuka Katiba, kanuni, maadili na nidhamu ya chama.

Kwa mujibu wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kufukuzwa huko kulimwondolea sifa ya kikatiba ya kuendelea kuwa makamu wa rais. Hivyo, safari iliyotarajiwa kumalizika Septemba 4 ikakatishwa Agosti 26.

Hapo ndipo kujiuzulu kukageuka kuwa jambo kubwa kuliko kujiuzulu. Kwa sababu swali halikuwa tena; Kwa nini Nchimbi amejiuzulu? Likawa; Nini hasa kimetokea?

### Barua yake inasema mengi

Katika barua yake, Nchimbi hakumtuhumu rais. Hakusema amefukuzwa serikalini. Hakusema amelazimishwa kujiuzulu.

Badala yake, alikumbusha ahadi aliyosema alimpa Rais Samia kabla ya uchaguzi wa 2025; kwamba angemsaidia kwa uaminifu, lakini siku rais akihitaji makamu mwingine, yeye angekuwa tayari kuondoka.

Kisha akaandika maneno ambayo ndiyo yamebeba uzito wa barua nzima: "Nimejiridhisha pasipo shaka kuwa Mheshimiwa Rais anatamani mabadiliko."

Akaondoka. Hapo ndipo lugha ya kisiasa inapotakiwa kusomwa zaidi ya maneno yenyewe.

Nchimbi hakusema rais alimwambia aondoke. Alisema yeye amejiridhisha kwamba rais anataka mabadiliko. Hakusema mabadiliko hayo ni yapi. Hakusema amejiridhisha kwa ushahidi gani.

Kwa hiyo, badala ya barua kujibu maswali, ikazalisha mengine. Kama huu ulikuwa uamuzi wa kawaida wa kustaafu, kwa nini CCM ilihitaji kumfukuza mtu ambaye tayari alikuwa ametangaza kuacha siasa?

Kama kosa lake lilikuwa kubwa kiasi cha kustahili kufukuzwa CCM, kosa hilo ni lipi? Na kama alikuwa amekiuka kwa kiwango hicho maadili na Katiba ya chama, ukiukaji huo ulianza lini?

Haya ndiyo maswali yanayofanya suala la Nchimbi lisimalizwe kwa taarifa ya kujiuzulu.

Inaendelea Uk. 21

Scanned with MOBILE SCANNER

# Kuondoka Nchimbi

Inatoka Uk. 20

**CCM inamjua Nchimbi**

Nchimbi hakuwa mgeni ndani ya CCM. Amekulia humo kisiasa. Amekuwa mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa CCM, mbunge, naibu waziri, waziri, balozi, katibu mkuu wa CCM na hatimaye makamu wa rais.

Huyu si mtu aliyekuja ghafla na chama kikashindwa kujua tabia yake, historia yake, marafiki zake, mitandao yake na fikra zake. Zaidi, Nchimbi ana historia ya kuwa na msimamo katika nyakati ambazo siyo rahisi kuwa nao.

Mwaka 2015 alikuwa miongoni mwa viongozi wa CCM waliopinga namna jina la Edward Lowassa lilivyoondolewa katika mchakato wa kupata mgombea urais wa chama.

Alipitia misukosuko yake, lakini hakutoweka. Miaka baadaye akarudi katika safu za juu, akawa Katibu Mkuu wa CCM.

Kisha akateuliwa kuwa mgombea mwenza wa Samia mwaka 2025. Hapo ndipo jambo linakuwa zito zaidi.

Kwa kumteua kuwa mgombea mwenza, CCM haikuwa inampa tu Nchimbi cheo. Ilikuwa inamweka katika nafasi ambayo, katika mazingira yanayotajwa na Katiba, inaweza kumfikisha kwenye urais. Tanzania tayari imeona hilo likitokea. Samia mwenyewe alikuwa makamu wa rais hadi Machi 2021, kifo cha Rais John Magufuli kilipomfikisha katika urais.

Kwa hiyo, chama kinapokuchagua kuwa mgombea mwenza, kwa maana nyingine kinakuwa kimesema; tumekuchunguza, tunakujua na tunakuamini kiasi cha kuwa tayari kukukabidhi nchi endapo mazingira yatahitaji. Ndiyo maana tukio la Nchimbi linahitaji maelezo zaidi. Mtu ambaye miezi michache iliyopita alifaa kuwa hatua moja kutoka urais, alikuwaje ghafla hafai hata kuwa mwanachama wa CCM?

**Labda tatizo ni nyendo zake**

Katika wiki zilizotangulia kuondoka kwake, Nchimbi alikuwa tayari amezua mjadala ndani na nje ya CCM kutokana na kauli zake kuhusu Katiba Mpya.

Julai 2026, akizungumza katika mkutano wa watetezi wa haki za binadamu, aliwataka Watanzania kuendelea kupigania Katiba Mpya; Katiba yenye muafaka wa kitaifa, inayoheshimu utu na haki za wananchi.

Kauli hiyo ilivuta mjadala mkubwa kwa sababu hoja ya Katiba Mpya tayari ilikuwa sehemu ya ahadi za serikali na CCM.

Lakini jambo muhimu zaidi halikuwa tu kile alichosema. Lilikuwa nani aliyesema hayo. Makamu wa Rais siyo mwanaharakati. Siyo kiongozi wa upinzani. Ni mtu wa pili katika uongozi wa nchi.

Anapowaambia wananchi "pambaneni" kupata jambo ambalo serikali yake yenyewe ina mamlaka makubwa ya kulitekeleza, sentensi hiyo inapata maana pana zaidi.

Watu wakaanza kuhoji; Pambaneni na nani? Hata Askofu Benson Bagonza aliuliza swali hilo wakati huo. Kama rais anataka katiba mpya, kwa nini wananchi waambiwe waipambanie?

Siwezi kusema kwa ushahidi kwamba kauli hiyo ndiyo iliyomwondoa Nchimbi. Lakini tunaweza kusema kwa uhakika kwamba ilizua mjadala na ukosoaji ndani ya chama.

Inaendelea Uk. 22



Dkt Emmanuel Nchimbi

Scanned with MOBILE SCANNER




# Kuondoka Nchimbi

Inatoka Uk. 21

Vyombo vya habari vimeripoti kwamba baadhi ya watu ndani ya CCM waliziona kauli zake kuwa hazikuwa za lazima. Hapo ndipo 2030 inapoingia.

**Kivuli cha 2030**

Tayari Nchimbi amekuwa anatajwa katika mijadala ya kisiasa kuwa anataka baada ya Samia. Kutajwa si kugombea. Kutamani si kutangaza nia. Na mpaka sasa hakuna ushahidi wa wazi kwamba Nchimbi alikuwa ameanzisha kampeni rasmi ya urais wa 2030.

Lakini siasa hazisubiri kampeni rasmi. Wakati mwingine tatizo la mwanasiasa si kile alichotangaza. Ni kile ambacho watu wenye mamlaka wanaamini anaweza kuwa anakifikiria.

Hapa ndipo nafasi ya .akamu wa rais inakuwa ya ajabu. Makamu anatakiwa kuwa mkubwa, lakini asiwe mkubwa sana. Anatakiwa kuonekana, lakini asionekane sana.

Anatakiwa kuwa na ushawishi wa kutosha kumsaidia rais, lakini ushawishi huo ukianza kuonekana kama mtandao wake binafsi, unaweza kuwa tatizo. Anatakiwa kuwa tayari kuwa rais ikibidi, lakini asionekane kama anasubiri kuwa rais. Hilo ndilo fumbo la umakamu wa rais.

Nchimbi mwenyewe alionekana kulifahamu. Alipokubali kuwa mgombea mwenza, alisisitiza hadharani kwamba angekuwa msaidizi, si mshindani wa Samia.

Kauli hiyo leo inavutia zaidi sasa kuliko ilivyokuwa wakati ilipotolewa.Kwa nini mtu ambaye hakutuhumiwa hadharani kumshindania rais aone umuhimu wa kusema yeye si mshindani?

Huenda ilikuwa lugha ya kawaida ya utii. Lakini huenda pia alikuwa anajua kwamba katika nafasi hiyo, hata uwezo wako tu unaweza kutafsiriwa kuwa tishio au ushindani.

**Kufukuzwa kwabadili simulizi**

Kama Nchimbi angeishia kujiuzulu na kwenda nyumbani, mjadala huu ungeweza kufa taratibu. Lakini CCM ikafanya jambo jingine. Ikamfukuza.

Katibu Mkuu wa CCM, Dk Asha-Rose Migiro, alisema vikao vya chama vilibaini ukiukaji wa Katiba, kanuni na maadili na kwamba uamuzi wa kumfukuza ulifikiwa kwa kauli moja. Lakini maelezo ya kina ya makosa yaliyosababisha adhabu hiyo hayajawekwa hadharani.

Kimsingi, CCM ndiyo ilifanya kesi ya Nchimbi kuwa kubwa zaidi. Kwa sababu sasa si suala la mtu kuamua kustaafu. Ni suala la chama kumwadhibu mtu ambaye jana yake alikuwa mtu wa pili kwa ukuu nchini.

Na adhabu hiyo ilikuwa na athari ya moja kwa moja ya kikatiba. Mwanasheria Mkuu wa Serikali amesema baada ya kupoteza uanachama wa chama kilichomdhamini, Nchimbi alipoteza pia sifa ya kuendelea kuwa Makamu wa Rais.

Kwa hiyo kufukuzwa hakukuwa ishara tu. Kulimaliza mamlaka yake.

Kwa hatua hiyo, Rais Samia sasa ana makamu mwingine: Deo Ndejembi. Kisiasa, hiyo inarudisha utulivu wa taasisi. Serikali inaendelea. Nafasi imejazwa. Mfumo unasonga mbele.

Inaendelea Uk. 23

Scanned with MOBILE SCANNER

# Kuondoka Nchimbi

Inatoka Uk. 22

Lakini uteuzi wa Ndejembi haujibu maswali yaliyoachwa na Nchimbi. Badala yake, unafungua mengine.

Ndejembi ameingia katika ofisi ambayo mtangulizi wake ameondoka katika mazingira ya kutatanisha. Atalazimika kujifunza mipaka yake mapema: kiasi gani cha kuonekana, kiasi gani cha kusema, kiasi gani cha kujenga ushawishi na, muhimu zaidi, jinsi ya kuwa mrithi wa kikatiba bila kuonekana kuwa mrithi wa kisiasa.

Hilo si tatizo la Ndejembi peke yake. Ni tatizo la mfumo. Kwa sababu kama makamu wa rais mwenye ushawishi anaweza kutafsiriwa kuwa tishio, basi mfumo unaweza kujikuta ukipendelea manaibu wasio na nguvu. Na makamu dhaifu anaweza kuwa salama kisiasa, lakini si lazima awe bora kwa nchi.

Nchimbi wa nje anaweza kuwa mkubwa kuliko wa ndani

Kuna uwezekano Nchimbi anamaanisha kabisa alichosema, kwamba amestaafu. Anaweza kwenda nyumbani na kukaa kimya.

Lakini mazingira yamembadilisha. Jana alikuwa mwanasiasa wa CCM aliyesema anastaafu. Leo ni makamu wa rais wa zamani aliyefukuzwa CCM. Hadi sasa hana chama.

Hayo ni mazingira mawili tofauti. Akiwa serikalini, alikuwa amefungwa na uwajibikaji wa pamoja. Akiwa CCM, alikuwa amefungwa na nidhamu ya chama.

Sasa minyororo yote miwili haipo. Hilo halimaanishi ataanza kuzungumza, lakini maana yake ni kwamba anaweza kuzungumza. Na akizungumza, atasikilizwa. Akinyamaza, ukimya wake nao utatafsiriwa.

Atakayetembelea nyumbani kwake ataangaliwa. Atakayemtetea ataangaliwa. Wanasiasa waliokuwa karibu naye wataangaliwa.

Na iwapo hatua za kinidhamu zitaanza kuwafuata watu wanaodhaniwa kuwa katika mtandao wake, tutajua kwamba jambo hili halikuwa kuhusu mtu mmoja, bali Lilihusu kitu kikubwa zaidi.

**Hilo si tatizo la Ndejembi peke yake. Ni tatizo la mfumo. Kwa sababu kama makamu wa rais mwenye ushawishi anaweza kutafsiriwa kuwa tishio, basi mfumo unaweza kujikuta ukipendelea manaibu wasio na nguvu.**

**2030 imeanza mapema**

Hapa ndipo kuna kejeli ya mwisho. Kama sehemu ya wasiwasi dhidi ya Nchimbi ilitokana na hofu kwamba alikuwa akijiandaa kwa 2030, basi kumwondoa kwake kumefanya jambo lilelile ambalo huenda lilikuwa linaogopwa.

Kumeanzisha mjadala wa 2030 mapema. Sasa kila anayepanda kisiasa atapimwa kwa kipimo hicho. Maswali yataibuka.

Rais Samia anataka nani baada yake? CCM inamwandaa nani? Ndejembi ni .akamu wa rais tu au anaweza kuwa zaidi? Nchimbi amestaafu kweli, au mazingira yanaweza kumrudisha?

Na kubwa zaidi: CCM itasimamiaje mpito wa madaraka baada ya Samia bila kugeuza kila mwanasiasa mwenye nguvu kuwa mshukiwa? Na katika mazingira ambayo CCM inazomewa kila kona, haitajiki walau mwanasiasa mmoja wa aina ya Nchimbi ambaye angesaidia chama kukubalika kwa umma na kushindana kwa hoja?

Haya ni baadhi ya maswali ambayo kuondoka kwa Nchimbi kumeacha mezani. Ndiyo maana simulizi hii haiwezi kufungwa kwa sentensi kwamba Emmanuel Nchimbi amejiuzulu umakamu wa rais au amefukuzwa uanachama. Hayo tunayajua.

Tusichokijua ndicho muhimu zaidi ni hiki; alifanya nini hasa, au mfumo uliamini alikuwa anakuwa nani, kiasi kwamba ndani ya muda mfupi mtu aliyekuwa anafaa kuwa hatua moja kutoka urais akaonekana hafai hata kubaki mwanachama wa chama kilichomfikisha huko?

Mpaka Nchimbi aamue kusema, au CCM iamue kueleza kwa undani zaidi, kuondoka kwake kutakuwa kumemaliza umakamu wake. Lakini hakutakuwa kumemaliza simulizi yake. Huenda ndiyo kwanza kumeanza.

Scanned with MOBILE SCANNER



Kilinge cha Mawasiliano

Na Loth MAKUZA

# Mabadiliko na kazi ya timu ya mawasiliano

OFISA mmoja wa mawasiliano alinipigia simu asubuhi baada ya kusambaa kwa taarifa kwamba Dkt. Emmanuel Nchimbi amefukuzwa ndani ya chama chake; CCM.

Hakutaka somo la historia kutoka kwangu. Alitaka kujua tu la kusema. "Tuwaambie nini watu?"

Baada ya zaidi ya muongo mmoja kwenye tasnia hii, naweza kukuambia hilo ndilo swali gumu kuliko yote niliyoyapata.

Kwa sababu mabadiliko ya uongozi kamwe siyo mabadiliko tu. Kiongozi wa juu anapoondolewa, kazi yetu sisi watu wa mawasiliano na umma hubadilika.

Watu wasipojua kilichotokea, huanza kubuni. Na kubuni hugeuka uvumi haraka, kwamba chama kinasambaratika, kwamba fulani ni mgonjwa, kwamba sera kubwa zinakaribia kubadilika. Uvumi hautulii.

Hivyo kazi ya kwanza ni kuzungumza mapema na kwa uwazi; ujumbe mmoja uliokubaliwa na wote, unaotolewa kabla habari potofu haijaenea. Hatuachi watu wauone kama ni "mgogoro."



Tunaueleza kwa maneno ya utulivu, serikali inajipanga upya ili ifanye kazi vizuri zaidi na kuwahudumia watu kwa haraka. Kunyamaza hakusaidii. Ukimya hutoa tu nafasi kwa uvumi kukua.

Lakini ujumbe mmoja hautoshi, kwa sababu mabadiliko ya uongozi hugusa makundi mengi kwa wakati mmoja, na kila kundi lina wasiwasi wa jambo tofauti.

Watumishi wa serikali wanataka kujua kama kazi zao ziko salama na kama maagizo yao bado yanasimama.

Viongozi wa chama wanahitaji kusema jambo lilelile, ili wasiwepo wawili wanaosema tofauti hadharani.

Wafanyabiashara na wawekezaji, ambao wanaweza kuyumbisha thamani ya fedha na bei kwa uvumi mmoja tu, wanahitaji kusikia kwamba mambo yako imara.

Washirika wa nje na balozi, ambao wamekuwa wakiifuatilia nchi hii kwa karibu tangu Oktoba iliyopita, husoma kila ishara.

Na umma, kundi kubwa na lisilo na subira kuliko yote, unahitaji ukweli ulio wazi kabla hadithi za kutunga hazijawafikia. Hivyo hatuwaambii wote kwa mara moja.

Tunawaambia watu wa ndani kwanza, ili taarifa ya hadhara inapotoka, asiwepo anayeshtukizwa.

Katikati ya haya yote, ni lazima pia tuonyeshe kisichobadilika. Nyuso ni mpya, lakini malengo, ahadi na mwelekeo havijabadilika. Na ni lazima tuseme haya kama binadamu wa kweli, siyo kama mashine, kwa maneno ya wazi na ya upole. Katika wakati wa wasiwasi, watu huamini ujoto wa moyo, si maneno makubwa. Watu wanaweza kukubali mabadiliko. Wasichoweza kukubali ni kuzungumzwa nao kana kwamba ni wapumbavu.

Kisha huja sehemu ambayo wengi husahau; mabadiliko ya uongozi si mwisho wa hadithi. Ni mwanzo wa hadithi nyingine. Siku thelathini za kwanza huamua kama watu watamkubali kiongozi mpya au watamvumilia tu.

Hivyo tunamtambulisha kwa uangalifu, siyo kwa kelele, ziara za mapema, mikutano ambayo yeye husikiliza zaidi kuliko kuongea, na jitihada za kweli za kujenga imani badala ya kuitegemea.

Pia tunaacha kuongea kutoka juu kwenda chini pekee. Tunawaruhusu watu wajibu, kupitia majukwaa ya wazi na maswali ya ukweli, na tunaendelea kufuatilia habari na hisia za watu, ili tuweze kujibu uvumi mdogo kabla haujakua moto.

***Mwandishi wa safu hii ni mtaalamu wa Uhusiano na Umma (PR). Anapatikana kwa namba: 0625 704 995 na kupitia email; projects@ lothmakuza.co.tz***

Scanned with MOBILE SCANNER



Na Emmanuel JACOB

Afya ya Kimwili

# Ni kweli watu wenye ulemavu hufichwa?

KATIKA jamii nyingi barani Afrika, ni nadra sana kuwaona watu wenye ulemavu wakijumuika kikamilifu kwenye maeneo ya umma.

Takwimu za kitaifa zinaonyesha kuwa nchini Tanzania kuwa takribani asilimia tisa hadi 11 ya wananchi wanaishi na aina fulani ya changamoto ya kiutendaji au ulemavu.

Tukiangalia idadi hii kubwa inabidi tujiulize; je, kweli tunawaona wakishiriki kikamilifu katika shughuli za kila siku za kijamii na kiuchumi, au wanaendelea kuachwa nyuma?

Kutokuonekana huku siyo kwa bahati mbaya, bali ni matokeo ya mfumo wa kijamii unaoendelea kuwatenga na kuwaficha ndani ya nyumba.

Mtazamo huu unachochewa na imani potofu za kiutamaduni pamoja na ukosefu wa miundombinu rafiki.

Wiki hii tunaangazia sababu ambazo zinasababisha watu wenye ulemavu kufichwa, ni muhimu kwa wasomaji wa safu hii wafahamu;

Kizuizi kikubwa kinachowafanya watu wenye ulemavu wakataliwe kuonekana hadharani ni unyanyapaa uliokita mizizi.

Katika jamii nyingi, ulemavu bado unahusishwa na ushirikina ukionekana kama laana, adhabu kutoka kwa mababu, au matokeo ya uchawi na dhambi zilizofanywa na familia.

Imani hizi huleta aibu kubwa kwa familia husika. Wasiwasi wa kupoteza heshima, kuharibu fursa za ndoa kwa wanafamilia wengine, na hofu ya kutengwa na jamii huwalazimisha wazazi au walezi kuwafungia ndani ndugu zao wenye ulemavu.

Badala ya kupewa fursa ya kuendelea, wanalazimika kuishi maisha ya kujificha ili kuepuka maneno ya kashfa na kutengwa na majirani.

Sababu nyingine ni zile zinazohusisha zaidi changamoto za miundombinu na uchumi;

Mbali na mtazamo wa kijamii, miundombinu isiyo rafiki inafanya ushirikishwaji wa watu wenye ulemavu kuwa ndoto isiyofikiwa.



Barabara nyingi, vyombo vya usafiri wa umma, majengo ya serikali na shule hazina njia za viti vya kulia (ramps), au alama za sauti kwa wenye ulemavu wa kuona na kusikia. Hali hii inamfanya mtu mwenye ulemavu kuwa mfungwa wa mazingira yake mwenyewe.

Umaskini pia unachangia kwa kiasi kikubwa. Vifaa saidizi kama viti vya kulia, magongo, au vifaa vya kusikia vina gharama kubwa ambazo familia nyingi hazimudu.

Bila msaada au ruzuku kutoka serikalini, familia zilizojikita katika umaskini hazina uwezo wa kutoa huduma hizi. Matokeo yake, huduma za afya na elimu zinabaki kuwa starehe badala ya haki ya msingi.

Ili kuondokana na hali hii ya unyanyapaa na ubaguzi, ni lazima jamii ibadili mtazamo wake. Ulemavu si laana wala aibu, bali ni utofauti wa kibinadamu unaohitaji fursa sawa.

***Mwandishi: Emmanuel Jacob, Afisa Mfiziotherapia (Mwenyekiti wa Tanzania Physiotherapy Initiative). Simu: 0765359305 Instagram: Emmanuel Jacob.***

Scanned with MOBILE SCANNER

Bustani ya Sheria



Na Wakili Karim Gabriel Mussa

# Sakata la Wakili Fatma Karume – VI

KATIKA sehemu ya tano tuliona jinsi Mahakama Kuu ilivyokataa kumpa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ruhusa (leave) ya kukata rufaa kwenda Mahakama ya Rufani dhidi ya uamuzi uliokuwa umemtendea haki Fatma Karume.

Lakini serikali haikuona huo kuwa mwisho wa safari. Iliamua kufanya kile ambacho wanasheria hukiita "second bite at the cherry." Yaani kuomba tena ruhusa, safari hii moja kwa moja mbele ya Mahakama ya Rufani.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na Kamati ya Maadili ya Mawakili waliwasilisha maombi mbele ya Mahakama ya Rufani.

Lengo lao lilikuwa lilelile. Kupewa ruhusa ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mahakama Kuu uliotengua uamuzi wa Kamati ya Maadili.


Kwa mtazamo wao, Mahakama Kuu ilikuwa imekosea kisheria, na walitaka Mahakama ya Rufani ichunguze makosa hayo.

Lakini Kabla hata hoja hizo hazijaanza kusikilizwa, kulijitokeza tatizo jingine; Pingamizi la kiufundi

Upande wa Fatma Karume uliweka pingamizi. Hoja ilikuwa kwamba maombi hayo hayakuwa yamekamilika kisheria, kwa sababu waombaji hawakuwa wameambatanisha Order (Amri) ya Mahakama Kuu waliyoitaka kuipinga.

Katika sheria za mwenendo wa mashauri, hati hiyo siyo jambo la hiari. Ni sehemu muhimu ya nyaraka zinazotakiwa kuambatanishwa ili Mahakama ijue rasmi uamuzi unaolalamikiwa.

Swali likawa hili; Je, kosa hilo lingeua maombi yote?



Mahakama ya Rufani ilikubaliana kwamba kulikuwa na kasoro ya kutokuwepo kwa Order.

Hata hivyo, Mahakama ya Tanzania ikaona kasoro hiyo ilikuwa inaweza kurekebishwa, badala ya kuua maombi yote mara moja.

Kwa msingi huo, Mahakama haikutupilia mbali maombi ya serikali. Badala yake, iliwapa waombaji nafasi ya kuwasilisha Order hiyo ndani ya muda waliopangiwa.

Kwa maneno mengine Mahakama ya Rufani ilichagua kutanguliza haki ya kusikiliza shauri badala ya kulimaliza kwa sababu ya kasoro iliyokuwa inaweza kurekebishwa.

**Kwanini uamuzi huu ni muhimu?**

Uamuzi huu ulikumbusha kanuni moja muhimu katika sheria za mwenendo wa mashauri.

Siyo kila kasoro ya kiufundi lazima iue shauri.

Pale ambapo kasoro inaweza kurekebishwa bila kuathiri haki za upande mwingine, Mahakama inaweza kutumia busara yake kuruhusu marekebisho badala ya kufunga mlango wa haki.

Ndiyo maana Mahakama ya Rufani haikusema serikali imeshinda, wala haikusema Fatma ameshinda.

Iliamua tu kwamba maombi ya serikali yaendelee kwa kufuata utaratibu sahihi, lakini wakati serikali Ikiendelea Kupambana, Fatma Karume naye alikuwa amefungua shauri lake tofauti kabisa katika Mahakama ya Rufani.

Safari hii hakupinga uamuzi wa Kamati ya Maadili, alikuwa anapinga uamuzi wa kwanza kabisa wa Jaji Feleshi uliomsimamisha kwa muda kufanya kazi ya uwakili.

Je, Mahakama ya Rufani ilikubaliana naye? Au ilisema alikuwa ametumia njia isiyo sahihi ya kuupinga uamuzi huo?

Hapo ndipo tunafika kwenye sehemu ya mwisho ya simulizi hili.

Itaendelea...

*Mwandishi ni Mwanasheria na Mchambuzi wa Sheria kutoka KGM Attorneys). Anapatikana kwa namba: 0755 395 572 au Email: karimbinmussa@gmail.com*

Scanned with MOBILE SCANNER





Na Rashid MTAGALUKA

Hoja Yangu

# Tusiipime serikali kwa kelele za mitandaoni



MITANDAO ya kijamii imebadilisha namna wananchi wanavyopokea na kutafsiri taarifa za serikali.

Leo, mtu anaweza kuamka asubuhi na kukutana na hoja nzito inayolenga serikali, taasisi au kiongozi fulani, na ndani ya muda mfupi hoja hiyo ikawa mjadala wa kitaifa. Hapa ndipo ninapoona serikali inahitaji kuwekeza zaidi katika mawasiliano ya umma.

Siyo kwamba, kila kinachoandikwa dhidi ya serikali ni uongo. Vivyo hivyo, siyo kila kinachoandikwa dhidi yake ni kweli.

Tatizo linakuja pale ambapo taarifa inapowekwa hadharani, serikali inachelewa kutoa ufafanuzi, huku wananchi wakiachwa wajijengee uelewa kupitia mitandao ya kijamii.

Mfano mzuri ni hoja mbalimbali zinazojadiliwa sasa kuhusu serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, zikiwamo suala la Tundu Lissu, matukio ya Oktoba 29, Katiba Mpya na madai kwamba serikali imejikita zaidi katika kushughulika na wapinzani kuliko matatizo ya wananchi.

Hoja hizi zinahitaji majibu, lakini si majibu ya hasira. Serikali inapokosolewa, jambo la kwanza siyo kumshambulia mkosoaji. Jambo la kwanza ni kujiuliza: Hoja hii ina ukweli kiasi gani? Tuna data gani? Na wananchi wanahitaji kujua nini?

Hapo ndipo mawasiliano ya serikali yanapokuwa muhimu. Serikali inapokuwa na taarifa sahihi, inapaswa kuzifikisha kwa wananchi kwa lugha rahisi na kwa wakati.

Inapokosewa, isisite kurekebisha taarifa. Inapokosolewa kwa jambo lenye msingi, ieleze hatua inayochukua. Na inapofanya vizuri, ieleze matokeo ya kazi hiyo badala ya kutegemea wananchi watajua wenyewe.

Mawasiliano mazuri siyo kuficha changamoto au kujibu kila mkosoaji. Ni kuhakikisha wananchi wanapata taarifa sahihi kuhusu kinachofanywa na serikali, sababu za hatua zinazochukuliwa na matokeo yanayopatikana.

Serikali inapoweka wazi taarifa zake, inapunguza nafasi ya uvumi, upotoshaji na tafsiri zinazoweza kupotosha uhalisia.

Kwa upande mwingine, wananchi nao wanapaswa kujifunza kutenganisha taarifa na propaganda. Si kila ujumbe unaosambaa kwa kasi ni ukweli, na si kila ujumbe unaoikosoa serikali unatokana na chuki.

Vyombo vya habari na waandishi nao wana wajibu wa kuchunguza taarifa, kuthibitisha takwimu na kutoa nafasi kwa pande zinazohusika kabla ya kujenga hitimisho.

Hoja Yangu wiki hii ni kwamba, tusiipime serikali kwa kelele za mitandaoni pekee. Wala tusiipime kwa sifa za wafuasi wake. Badala yake, tuipime kwa kazi inayofanya na namna kazi hiyo inavyobadili maisha ya wananchi.

Aidha, tuipime kwa huduma zinazowafikia wananchi, kwa ajira zinazopatikana, kwa ubora wa elimu na afya, kwa maji, nishati na miundombinu. Tuipime pia kwa uwezo wake wa kusikiliza wananchi, kukubali pale inapokosea na kurekebisha pale inapobidi.

Kwa sababu hatimaye, serikali haipaswi kuogopa ukosoaji. Ukosoaji wenye hoja unaweza kuwa kioo kinachoonesha maeneo yanayohitaji kurekebishwa.

Serikali bora ni ile inayoweza kusikiliza ukosoaji, kujibu kwa ukweli, kujirekebisha inapobidi na kuendelea kufanya kazi.

***Rashid Mtagaluka ni mwandishi wa habari na anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gm .com***

Scanned with MOBILE SCANNER

## Habari

# Padre aadhimisha misa juu ya Mlima K'njaro



Na Mwandishi WETU

MLIMA Kilimanjaro umezoeleka kwa shughuli za utalii pekee, lakini tukio la hivi karibuni limeupa mlima huo mrefu kuliko yote Afrika taswira mpya katika ramani ya utalii wa Tanzania.

Tukio hilo linaonyesha kuwa Mlima Kilimanjaro siyo tena eneo linalovutia wanaopanda milima na wapenda mazingira pekee, bali eneo hilo linaweza pia kuwa jukwaa la utalii wa kiimani - mchanganyiko unaoweza kuongeza thamani ya moja ya vivutio vikubwa zaidi vya nchi.

Jambo hilo limejirudia mwaka huu kupitia hija ya Padre João Silveira, Mmisionari Mkatoliki kutoka Ureno, aliyeshiriki safari ya siku nane kuupanda mlima huo kupitia njia ya Lemosho na kuadhimisha Misa ya Jadi ya Kilatini katika safari hiyo, ikiwamo katika kilele cha Uhuru Peak, mita 5,895 juu ya usawa wa bahari.

Taarifa za waandaaji wa hija zinaonyesha kuwa safari hiyo iliyofanyika mwezi uliopita – Agosti, ilihusisha sala, Misa ya Kilatini na kupanda mlima, huku waumini wakitumia safari hiyo kama hija ya kiroho na pia kuunga mkono kazi za kimisionari Tanzania.

Padre kuadhimisha misa akiwa madhabahuni ni tukio la kawaida, lakini misa hii ilioyoadhimishwa katika kilele cha mlima unaonyesha utafauti mkubwa ukitoa picha ya padre akiwa madhabahuni juu ya mlima wa kitalii.

Kilimanjaro ni moja ya maeneo ya Urithi wa Dunia yanayotambuliwa na Unesco. Ni mlima mrefu kuliko yote Afrika.

Mamlaka ya Hifadhi za Taifa (Tanapa) inautaja pia kuwa mlima mrefu zaidi duniani usiosimama peke yake (usiokuwa katika safu ya milima).

Takwimu kutoka Wizara ya Maliasili na Utalii zinaonyesha kuwa Mlima Kilimanjaro ulipokea zaidi ya wageni 58,000 wa kimataifa mwaka 2024.

Wakati huohuo, ukanda wa utalii wa kaskazini, unaojumuisha Mlima Kilimanjaro, hifadhi za Serengeti na Ngorongoro, uliendelea kuwa kitovu kikubwa cha mapato ya utalii nchini.

Hivyo, hija kama ya Padre Silveira inaweza kutazamwa kama sehemu ya mabadiliko mapana ya namna Tanzania inavyoweza kukuza sifa za utalii za Mlima huu, kwani tukio hili linaweza kuanzisha safari ya kuufanya mlima huu kuwa eneo la hija (hata kama halitatambuliwa rasmi) kwa waumini wa Kikatoliki kutoka maeneo mengi duniani.

Muhimu zaidi, tukio hili linaonyesha kuwa utalii wa kiimani unaweza kuunganishwa na bidhaa nyingine za utalii badala ya kutazamwa kama shughuli inayojitegemea.

Hija inaweza kuhusisha malazi, usafiri, wapagazi, waongoza watalii, chakula, huduma za afya na shughuli za kitamaduni kabla na baada ya kupanda mlima.

Historia yenyewe inalifanya tukio hili kuwa zito zaidi tangu Johannes Rebmann, mmisionari Mjerumani, alipouona na kuripoti uwepo wa Kilimanjaro mwaka 1848.

Zipo taarifa kuwa Rebmann aliadhimisha Misa kileleni wakati huo, lakini taarifa hizo bado hazijapata uthibitisho.

Aidha, Misa zimewahi kuadhimishwa kileleni na mapadre wengine, akiwamo Fr. Corwin Low mwaka 2022 na Fr. Antony Sumich pamoja na Fr. Gregory Bartholomew mwaka 2015.

Tukio hili linathibitisha kuwa Mlima Kilimanjaro bado ina bidhaa mpya za utalii ambazo hazijatumika kikamilifu.

Scanned with MOBILE SCANNER




Scanned with
MOBILE SCANNER

## Barua za Wasomaji



**Tunakaribisha barua. Tuma kupitia**

**Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba; +255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@pambazuko.or.tz**

# Serikali idhibiti wanawake wanaouza miili yao

**Mhariri,**

NAKERWA na kukithiri kwa wanawake wanaouza miili yao katika miji yetu hasa nyakati za usiku.

Jambo hili limekuwa tatizo kubwa kwa wanawake na hivi sasa wasichana wenye umri mdogo wengi wao kuanzia miaka 18 hadi 22 ambao ndio nguvu kazi ya taifa wanashiriki kwenye vitendi hivi wakidhani kwamba watarahisisha maisha kwa kupata fedha kwa haraka.

Mhariri, madhara ya jambo hili ni makubwa mojawapo ni kuweka afya zao rehani kwa kupata uwezekano wa magonjwa za ngono vikiwemo virusi vya Ukimwi.

Naiomba serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kudhibiti biashara hii ili isizidi kuenea.

**Amina Juma**
**Dar es Salaam**

# Wapiga debe wamekuwa kero zaidi

**Mhariri,**

TATIZO la wapiga debe katika miji mikubwa linasumbua abiria katika vituo mbalimbali vya mabasi. Tatizo hili limekuwa kero kwa abiria hasa katika Jiji la Dar es Salaam.

Ukiwa kituoni wapiga debe hao wamekuwa wakipiga kelele na kuleta usumbufu kwa abiria kwa lugha chafu.

Vituo kama Ubungo, Kariakoo na Mabibo vimekuwa kero kwa tabia hizo kwa sababu ya tabia chafu ya wapiga debe.

Abiria wengi wanachelewa kazini na wengine wanaacha kupanda magari kwa hasira kutokana na adha ya wapigadebe

Shime kwa Halmashauri iweke utaratibu wa kukagua vituo mbalimbali vya abiria ili kuwadhibiti.

**Rebecca Saimoni,**
**Ubungo,**
**Dar es Salaam**

# Mazingira machafu eneo la Gerezani yatutesa

**Mhariri,**

NAKUANDIKIA barua hii kwa masikitiko kuhusu tatizo la maji machafu yanayotiririka katika eneo la Gerezani, Kariakoo.

Kwa miezi kadhaa sasa mifereji ya eneo hilo imeziba huku maji ya vyooni na taka za viwandani yakipita na kusambaa barabarani.

Hali hiyo imekuwa ikitutesa kutokana na harufu kali ambayo wakati mwingine watu waliopo katika mazingira hayo wamekuwa wakishika pua.

Mbali na hilo, tatizo hili pia linaathiri afya zetu jambo ambalo linaweza kutishia magonjwa ya kuhara, kipindupindu na magonjwa ya ngozi lakini pia kibiashara wateja wengi wanaogopa kuja kununua katika maeneo yetu kwa sababu ya uchafu.

Kwa upande wa mazingira, barabara zimeharibika kwani mvua kidogo ikinyesha eneo lote linakuwa bwawa la uchafu.

Tunaomba mamlaka husika walishughulikie kero hii ili kuondoa hali hatarishi.

**Amina Hassan,**
**Mbagala, Dar es Salaam**

Scanned with MOBILE SCANNER




Scanned with MOBILE SCANNER

## Makala

# Pengo elimu afya ya uzazi tishio ustawi wa vijana - II



Na Elizabeth MWINUKA, Dodoma

KATIKA sehemu ya kwanza ya makala haya tuliona jinsi ukosefu wa elimu sahihi ya afya ya uzazi unavyoathiri makundi ya vijana katika Mkoa wa dodoma.

Wengi hudhani kuwa hali kama hiyo huwaathiri tu vijana ambao hawana elimu kubwa, lakini uchunguzi wa gazeti hili umebaini kuwa hata vijana wenye elimu kubwa nao wameathirika na hali hiyo.

Katika Chuo Kikuu cha Dodoma hali haikuwa tofauti.

Wanafunzi waliozungumza na mwandishi wa Makala haya walisema elimu ya afya ya uzazi hupatikana zaidi kupitia makongamano na semina zinazoratibiwa na wadau mbalimbali, lakini washiriki ni wachache.

Mwanafunzi mmoja wa UDOM anasema; "Mara nyingi wanaopata nafasi ni viongozi wa wanafunzi au waliopo kwenye Klabu za Jinsia (Gender Club). Wanafunzi wengi hawafiki kabisa."

Wanafunzi wengi wanasema kuwa hali hiyo imewafanya vijana wengi kutegemea taarifa kutoka kwa marafiki na mitandao ya kijamii kuliko wataalamu wa afya.

Wataalamu wa afya wanaonya kuwa pengo la elimu ya afya ya uzazi lina athari zinazozidi mimba za utotoni pekee.

Pengo hilo pia linaongeza maambukizi ya magonjwa ya zinaa, changamoto za afya ya akili, utoaji mimba usio salama pamoja na kusitishwa kwa masomo kwa baadhi ya vijana.

**Dodoma matokeo hayaonekani**

Serikali kupitia Mpango wa Kitaifa wa Uzazi wa Mpango (National Family Planning Costed Implementation Plan; 2019–2023) inautaja Mkoa wa Dodoma kuwa miongoni mwa maeneo ya kipaumbele katika kupanua elimu ya afya ya uzazi na kuongeza upatikanaji wa huduma za uzazi wa mpango.

Hata hivyo, uchunguzi huu unaonyesha vijana katika Makulu, Iyumbu, Ntyuka, Ng'ong'ona na hata Chuo Kikuu cha Dodoma bado wanategemea kampeni za muda mfupi kupata elimu ya afya ya uzazi badala ya kuwa na mfumo endelevu wa elimu.

Daktari mmoja anasema; "Elimu ya afya ya uzazi siyo elimu ya kuzuia mimba pekee, ni elimu ya kumwezesha kijana kufanya uamuzi sahihi kuhusu mwili wake, afya yake na maisha yake."

Mahojiano ya wadau mbalimbali yamebainisha kuwa changamoto kubwa siyo ukosefu wa sera wala sheria kwa kuwa zipo.

Inaendelea Uk. 33

Scanned with MOBILE SCANNER

# Pengo elimu afya...

Inatoka Uk. 32

Tanzania imekuwa na Sheria ya Afya ya Umma ya mwaka 2009, Sheria ya Kudhibiti VVU na Ukimwi ya mwaka 2008 pamoja na National Adolescent Friendly Health Services Guidelines zinazotaka vituo vya afya kutoa huduma rafiki kwa vijana.

Miongozo hiyo inasisitiza huduma zinazolinda faragha, utu na usiri wa vijana.

Hata hivyo, uchunguzi huu unaonyesha kuwa utekelezaji wa matakwa haya ya kisheria bado una upungufu mkubwa.

Kwa nchi inayotarajia kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050, kuendelea kuwaacha vijana wakitegemea taarifa kutoka kwa marafiki na mitandao ya kijamii kuhusu afya ya uzazi kunaweza kuwa na gharama kubwa zaidi kuliko inavyoonekana leo.

**Gharama za ukimya**

Madhara ya pengo hili hayaishii kwenye mimba za utotoni pekee.

Takwimu za kitaifa zinaonyesha Tanzania bado inapoteza wastani wa akina mama 233 kwa kila vizazi hai 100,000. Wataalamu wanaeleza kuwa vijana waliopata ujauzito bila maandalizi huwa katika kundi lenye hatari kubwa ya kupata matatizo ya uzazi.

Aidha, Sensa ya mwaka 2022 inaonyesha kuwa asilimia 63.2 ya wasichana wa vijijini wenye umri wa miaka 15 hadi 17 waliopata ujauzito hulazimika kuacha shule, jambo linalopunguza fursa zao za elimu na kipato.

Ushahidi uliokusanywa katika maeneo mbalimbali ya Jiji la Dodoma unaonyesha kuwa changamoto kubwa si ukosefu wa sheria wala sera. Tatizo ni kushindwa kuzitekeleza kwa kiwango kinachoweza kuwafikia vijana wote.

Wakati vijana ni zaidi ya theluthi moja ya wakazi wa Mkoa wa Dodoma, zaidi ya asilimia 60 bado wana uelewa mdogo wa afya ya uzazi, huku karibu msichana mmoja kati ya watatu akiwa tayari amewahi kupata ujauzito.



Takwimu hizi zinaonyesha kuwa gharama ya kutowekeza katika elimu ya afya ya uzazi si ya mtu mmoja mmoja, bali ni ya jamii na taifa kwa ujumla.

Bila mfumo endelevu wa elimu, huduma rafiki kwa vijana na uwajibikaji wa viongozi katika kusimamia utekelezaji wa sheria zilizopo, Dodoma itaendelea kupoteza kizazi cha vijana kinachopaswa kuwa nguvu kazi ya maendeleo.

**Tuendako**

Ushahidi uliokusanywa katika Jiji la Dodoma kupitia mahojiano na watu mbalimbali unaonyesha kuwa changamoto haipo katika ukosefu wa sheria wala sera, bali katika pengo la utekelezaji.

Wakati takribani msichana mmoja kati ya watatu tayari amewahi kupata ujauzito na zaidi ya asilimia 60 ya vijana wakionyesha uelewa mdogo kuhusu afya ya uzazi, wataalamu wanaamini suluhisho linahitaji elimu endelevu, huduma rafiki kwa vijana na uwekezaji wa muda mrefu badala ya kampeni za msimu.

Bila hatua hizo, pengo la elimu ya afya ya uzazi litaendelea kuzalisha kizazi kinachoingia utu uzima bila taarifa sahihi za kufanya uamuzi unaogusa afya, elimu na mustakabali wa maisha yao.

***Mwandishi ni mwanafunzi wa shahada ya uandishi wa habari katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).***

Scanned with MOBILE SCANNER



Na Anti MSHAURI



# Mabinti lindeni thamani yenu

HABARI za leo msomaji wa safu hii ya uhusiano na karibu uweze kujipatia elimu na ujuzi mbalimbali wa masuala ya maisha.

Wiki iliyopita nilizungumza umuhimu wa kumtanguliza Mungu mbele kwenye kila jambo unalofanya na wiki hii nitazungumza umuhimu wa binti kujua thamani yake.

Binti anapaswa kutambua thamani yake ili aweze kujenga maisha yenye mwelekeo na mafanikio.

Thamani ya binti haipimwi kwa kupendwa na wanaume wa aina tofauti au kwa namna nyingine, bali kwa kujithamini.

Katika zama za sasa mabinti wengi wamekuwa wakitumia njia za mkato pale wanapotongozwa na wanaume hasa wenye umri mkubwa 'mashuga dadi' na kuamua kujenga uhusiano nao na kusahau kuwa kufanya hivyo kunawachelewesha kutafuta maisha yao ya baadaye ya kujenga familia zao na maisha kwa ujumla.

Mabinti hao huanzisha uhusiano na wanaume hao ambao huwarubuni kwa kuwapatia zawadi kama simu, pesa na anasa ili washawishike kuwa nao na waingiapo hujichia wakati mwingine kuzaa nao.

Hali hiyo huwafanya wengi kupumbazwa na uhusiano huo usio na faida na mwisho wa siku huwafanya kushindwa kutengeneza maisha yao ya baadaye.

Kutokana na kujiingiza huko kwenye uhusiano usio na msingi na wanapotelekezwa hubaki wakilea kwa changamoto watoto waliopewa na wanaume waliokuwa na uhusiano nao na kubaki wakijuta.

Wengine hujitumbukiza kwenye uhusiano huo wakiwa shuleni na baadaye kujikuta wakipoteza masomo na muda wao.

Wengi wao hujitumbukiza kwenye mambo hayo kwa kufuata mkumbo(kuiga) kutoka kwa wengine na kusahau kuwa mwisho wa mambo hayo huwa ni mbaya.

Binti kabla hajafikia kutaka kufanya jambo lolote anatakiwa kuwa na maamuzi yake binafsi kutafakari na kufikiri kwa undani kuhusu faida na hasara zake.

Ili kutojiweka kwenye misukosuko binti anatakiwa kuepuka shinikizo lolote la marafiki au kuingia tamaa za muda mfupi katika kupata kitu fulani pia kufikiri na kuwa na uamuzi wa kukubali jambo linalomfaa na kulikataa lisilomfaa kwani hali hiyo itamsaidia kutimiza ndoto zake njema.

Binti akumbuke kuwa uamuzi wake binafsi ndiyo njia pekee inayoweza kumpatia nguvu ya kujisimamia na kujipanga bila kutegemea mtu mwingine.

Wazazi, walimu na jamii wana wajibu wa kuwakumbusha mabinti kila wakati kuhusu thamani yao na namna ya kuilinda na kujiheshimu.

Wakielewa na kujiheshimu, hawatapoteza wakati bali watajenga kesho yao iliyo bora.

Tukutane wiki ijayo.

*Kwa maoni na ushauri: hellen2ngoromera@gmail.com Au simu: 0715 88 67 49.*

Scanned with MOBILE SCANNER

# Adolphine, mumewe walivyotikisa kwenye vazi la asili la harusi

MWANAMITINDO na mjasiriamali, Adolphine Manywa, akiwa na mwenza wake wameteka hisia za wengi baada ya kuonekana wakiwa kwenye mavazi ya kipekee ya harusi ya asili.

Wawili hawa wameleta mapinduzi makubwa kwa kuchanganya utamaduni wa mwafrika na ubunifu wa kisasa uliowafanya waonekane kama mfalme na malkia kamili.

Bibi harusi amevaa gauni la lililopambwa kwa ushanga wa asili. Gauni hilo lina muundo wa ngozi ya ng'ombe kwenye sehemu ya kifuani na chini.

Amekamilisha muonekano wake wa malkia kwa kofia ya asili ya kusuka iliyopambwa pamoja na pepeo la mkononi lililotengenezwa kwa ngozi ya ng'ombe.

Kwa upande wa bwana harusi, amevaa suti ya rangi ya cream iliyowekwa kipande cha ngozi ya ng'ombe kifuani upande mmoja kinachoendana kabisa na gauni la bibi harusi.

Akaongeza na nakshi za kifalme kwa kuvaa kofia ya crown ya ngozi ya ng'ombe, miwani nyeusi, pamoja na bakora ya mfalme iliyochongwa kwa mti mweusi.



Scanned with MOBILE SCANNER





# Gwajima: Mungu ameweka kitu kwa Dudubaya, aache matusi

Na Mwandishi WETU

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dkt. Dorothy Gwajima, amesema msanii Dudubaya ana kitu ambacho amepewa na Mungu na endapo ataacha matusi kitu hicho kitaza faida kubwa.

Dkt. Gwajima ametoa kauli hiyo wakati akihojiwa kuhusu kauli ya Dudubaya ambayo anapenda kuitumia ya 'you better watch your back' akimaanisha linda mgongo wako.

Waziri huyo amesema ni jambo zuri kwa msanii huyo kufanya kampeni ya kupinga ushoga na usagaji.

Hata hivyo, Dkt. Gwajima amemtaka Dudubaya kutumia lugha nzuri na yenye kujenga katika kufikisha ujumbe wake, akieleza kuwa anaweza hata kupewa nafasi ya kuwa balozi wa kampeni hiyo.

"Hakuna mtu aliyekamilika duniani, Dudubaya akiacha matusi ana kitu kikubwa ambacho Mungu kamjalia," amesema Gwajima.

# Diamond kuachia albamu mpya Oktoba

Na Mwandishi WETU

MSANII Diamond Platnumz amesema ataachia albamu yake mpya Oktoba mwaka huu, ikiwa ni miaka minane tangu alipotoka na A Boy From Tandale mwaka 2018.

"Baada ya miaka nane sasa naenda kuachia album nyingine. Inaweza kutoka Oktoba 2, sijui, lakini album inakuja na collabo kubwa, sound kubwa na muziki mzito," amesema Diamond.

Ameeleza kuwa ukimya wake wa hivi karibuni haukuwa wa bahati mbaya, bali alikuwa akijikita zaidi katika kuandaa album hiyo.



MOBILE SCANNER




# Steven Gerrard atia neno Liverpool

Na John MARWA

NYOTA wa zamani katika klabu ya Liverpool, Steven Gerrard amesema klabu hiyo imeanza msimu kiulaini mno hali inayotishia kutokuwa na makali ya kuwania taji la Ligi Kuu ya England msimu huu.

Kufuatia kusuasua kwa safari yake ya ushindi, amemtaka Kocha Andoni Iraola kuongeza wachezaji wakatili katika maeneo muhimu.

Kauli ya Gerrard imekuja mara baada ya kutoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Nottingham Forest Jumamosi iliyopita katika Dimba la Anfield.

"Nadhani Liverpool hii ni timu laini mno. Hawana mtu wa kuharibu mipango ya timu pinzani, atakayeshinda mapambano na mzuri uwanjani..."

"Hivyo wanapaswa kupata mtu katili ndani ya uwanja ambaye atailinda timu na kuifanya kuwa salama kutekeleza mpango kazi wa kupata matokeo kwenye michezo yao," alisema Gerrard akiambia TNT Sports na kuongeza kuwa.

"Kuna muda unashinda mchezo kwa njia tofauti, kikosi kina wachezaji wazuri sana kimbinu na wenye vipaji lakini kinakosa mtu wa kazi, nadhani kocha anajukumu la kumpata huyo mtu aje kuisaidia timu.

"Vinginevyo kama hawatapata mtu wa kuja kuifanyia timu kazi ngumu katikati ya uwanja sio rahisi kushinda taji, mwishoni mwa msimu hawatashinda chochote zaidi ya kuwa watazamaji.

Liverpool wamecheza michezo miwili sawa na dakika 180 wakitoka sare michezo yote, dhidi ya Newcastle 2-2 na dhidi ya Nottingham Forest 2-2. Pointi mbili, nafasi ya 11 kwenye msimamo wa EPL.

Scanned with MOBILE SCANNER



# Dakika 360 za kibabe kwa Simba, Yanga



Cheikh Touré

Na John MARWA

DAKIKA 360 za Ligi Kuu Soka ya NBC PL 2026/27 zimetimia kwa kila klabu kucheza michezo minne, huku maji na mafuta vikianza kujitenga katika safari ya kuwania ubingwa wa Tanzanzia Bara msimu huu.

Klabu za Simba na Yanga zimeanza kwa kishindo kizito msimu huu, kwa kila timu kupata ushindi wa asilimia miamoja za michezo hiyo minne, na kuwasha taa ya kijani ya kuwania taji, umande ukiwa haujakauka.

Wananchi Yanga ambao ni mabingwa watetezi, wamevuna pointi 12 katika dakika 360, dhidi ya Namungo FC, Coastal Union, JKT Tanzania na Pamba Jiji FC, wakifunga mabao 13 na kuruhusu mabao 2, na kuwa nafasi ya kwanza kwenye msimamo.

Wakati huo Mnyama Simba akivuna pointi 12 kwenye michezo minne sawa na watani zao ambapo, amewapepeta Kagera Sugar, Pamba Jiji FC, Singida Black Stars na Coastal Union, mabao 7 ya kufunga huku wakiruhusu mabao mawili, nafasi ya pili kwenye msimamo kwa tofauti ya mabao ya kufunga.

Kwa namna miamba hiyo ilivyoanza ligi ni wazi vita ndio vimeanza upya licha ya Wananchi kutamba katika misimu mitano mtawalia, huu ukiwa wa sita ambapo Mnyama ana kazi ya kujiuliza kama atarejesha ufalme wake msimbazi kwa kunyanyua taji hilo.

Swali ni je, ni Simba ama Yanga atakayedondosha alama msimu huu kwa kupata, suluhu, sare ama kupoteza? Wakati tunasubiri majibu katika mahakama ya muda, Azam FC wao wamerejea kwenye maisha yao ya kawaida ya kushindwa kutamba ugenini.

Ni kama mzimu wao hauna furaha kabisa wakiwa katika viwanja vya mikoani, Azam, wamecheza dakika 360, dakika 180 sawa na michezo miwili ya ugenini dhidi ya Polisi Tanzania na Geita Gold zote wameambulia sare.

Katika alama 12 tayari wameangusha alama 4, sawa na asilimia 33.33 za pointi walizopoteza, wakishika nafasi ya nne nyuma ya Mbeya City wenye pointi tisa, wakishinda michezo mitatu na kupoteza mmoja.

*GAZETI hili lilianzishwa 2021, kuandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa) na kusajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448. Linaendeshwa kwa ushirikiano wa mzunguko – kwa kila nchi, wa mwaka mmoja na waandishi wa Tanzania, Kenya, Uganda, DRC na Rwanda.*

Scanned with
MOBILE SCANNER